# Kufanywa Wana Wenye Mamlaka #3

Jeffersonville, Indiana, USA

Mei 22, 1960

1 … Neville. Habari za asubuhi, darasa. Tuna furaha sana kurudi tena tupate kuwasalimu tena katika Jina hilo litoshelezalo kabisa la Bwana Yesu. Tukitumaini ya kwamba mmekuwa na wiki nzuri sana ya sifa na baraka Zake.

Nilipoingia tu asubuhi ya leo, nilikutana na mvulana mdogo pale naye akanipa salamu ndogo ya Malaika mlinzi akiwalinda watoto wawili wadogo. Nami sikujua ya kwamba huyo alikuwa wa Daulton, mvulana mdogo wa Daulton.

2 Na hapa majuma machache yaliyopita, ama ninii chache … Yapata majuma mawili yaliyopita, kulikuwako na baba fulani, baba Mkristo, aliomba kwa ajili ya binti yake tineja ambaye hakuwa Mkristo bado, wakati alipokuwa amesimama kwenye mstari wa maombi. Naye Roho Mtakatifu akasema, "Na—nakupa mtoto wako." Naye ndiye huyu hapa asubuhi ya leo, ameokolewa na kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu, ameketi jukwaani, kama tu vile Roho Mtakatifu alivyosema. Na hao watoto wengine wote wameketi hapa. Najua familia ya Daulton inayo furaha.

3 Namwona yule bibiye mdogo pale ambaye walimwombea mtoto wake mchanga Jumapili iliyopita, walidhani atakufa. Naona kwamba yungali pamoja nasi asubuhi hii, nasi tuna furaha sana kwa ajili ya jambo hilo, dada. Walidhani ilikuwa na ugonjwa wa unyonge wa misuli, naye hakuwa nao. Kwa hiyo tunashukuru sana.

4 Nawaona marafiki wetu wote walio wazuri. Namkumbuka mtu huyu hapa akinijia katika mahojiano maalum kule—huko Chautauqua wakati mmoja, naamini ilikuwa huko. Nilikuwa na kiamshakinywa pamoja na wewe na mke wako na watoto, naamini … ama wewe na mkeo, ama watoto, naam, pia. [Ndugu fulani anasema, "Middletown." — Mh.] Middletown, kwenye … Lakini sisi sote … Ninasahau jina hilo, kwa hiyo ninapaita tu Chautauqua. Naam, bwana. Wengi wa marafiki zangu wazuri.

Ndugu Charlie Cox na Dada Nellie hapa, ambao wamekuwa nyumba ya pili kwangu, na hakuna lingine ila niyi mngeweza kuwa watoto wangu mwenyewe. Nashuka kwenda kule, ndiko ninakotumia muda wangu mwingi wa kupumzika, ni kule chini. Yeye ndiye mwindaji bora zaidi wa kindi katika Kentucky ninapokuwa Indiana. Na kwa hiyo Indiana … Na Charlie, nakwaambia ninatamani tu, nikijisikia sana kama inanipasa kuwashika hao samaki wakubwa wachache pamoja au wenye milia kabla sijaanza kuingia kule. Kwa kweli ninajisikia tu kama ningeweza kustahimili hilo sana.

5 Ndugu Parnell … Par- … Arnett, kutoka Lou- … Carolina ya Kusini. Na Ndugu … Vema, ni watu wengi tu tofauti hapa kutokea mahali mbalimbali, waliokuja asubuhi hii kututembelea.

Unajua, hatuna wafuasi waliojiandikisha hapa. Tuna ushirika sisi kwa sisi, huku Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatutakasa na udhalimu wote.

6 Sasa, tuna somo zuri sana, tukufu tu. Nasi tunaninii, angalau mimi … najua ninalifurahia, nami najua ninyi nyote mnalifurahia pia. Ninaanza wakati mwingine siku nzima, kulizungumzia ama kulisoma nachukua kama aya mbili na ninaanza kupitia Maandiko na, muda si muda, tayari nimetoka Mwanzo hadi Ufunuo, nikiendelea.

Na, mnjua, ningetaka kuchukua wakati ambapo tungeweza—ambapo tungeweza kuingia kwenye Kitabu cha—cha Waebrania, na kuchukua kama tu … Vema, wakati msimu wa kindi unapoingia, kama Septem- … kwenye Okt- … Agosti, mwajua, na kuendelea hadi wakati wa kwenda nchi za ng'ambo, kila usiku tu kwenye Kitabu cha Waebrania, ama Kitabu cha Kutoka. Jinsi ambavyo Mungu, Kutoka, akiwatoa watu Wake kutoka Misri, kutoka! Mfano mzuri sana wetu sisi tunapojitayarisha kwa ajili ya kutoka kwetu. Ni, loo, ni jambo zuri sana. Maandiko yote yanaungana tu, na ni Habari moja kubwa.

7 Sasa, asubuhi ya leo tungali—tungali katika Kitabu cha … Tulikuwa tuzichukue sura tatu za kwanza za—za Kitabu cha Waefeso. Waraka wa Paulo kwa Waefeso huko Efeso, akijaribu, kuliweka kanisa mahali pake. Na kabla tu hatujaliendea, tungeweza tu kuchukua dakika moja ama mbili kwa ajili ya maombi, kabla tu hatujafanya hivyo.

8 Ee Bwana, Mungu wetu, tunakuja katika Uwepo Wako sasa, vivi hivi tukiwa hatustahili, hata hivyo tunajua ya kwamba kuna Dhabihu ya Damu pale ikingojea, ikitusafisha na uchafu wote, na kutuwakilisha mbele za Baba, tusio na hatia, tusio na kosa. Hakuna kitu tunachoweza kufanya kustahili jambo hili. Lakini kwa sababu ya kwamba Yesu amefanya jambo hili kwa ajili yetu, tunainamba kwa unyenyekevu kwenye Uwepo Wake na Jina Lake, tukiomba kwamba utamtuma Roho Mtakatifu asubuhi ya leo katikati yetu. Na kwa kuwa mimi si mwanatheolojia ama sijui jinsi ya kuweka Maandiko katika utaratibu, bali ni mwenye shauku na shukurani kwenye kumhisi Roho Mtakatifu anapotembea ndani ya utu wangu, hebu atubariki sisi sote pamoja tunaposoma Neno Lako lililoandikwa, ili kwamba Hilo liweze kufanyika kwetu Uzima wa Milele. Tujalie, Baba. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu na kwa ajili ya Yesu. Amina.

9 Sasa ningesema hapa ndani, kwanza, kwamba kama wakati wowote ningeweza kusema jambo ambalo lingekuwa halikubaliki, kutoliweka vizuri, labda haliambatani kabisa na mafundisho yenu, ama jambo fulani ambalo usingeweza kukubaliana nalo, ninamtumainia Roho Mtakatifu, ya kwamba atalifanya likolee sana na liwe tamu sana hata hakutakuwa na … halitaudhi hata kidogo. Unaona? Kwamba ita—itakuwa ni kwa upendo na ushirika, kwamba hiyo ndiyo … Limekusudiwa hivyo.

Na haya yote yalianza na mahubiri Jumapili iliyopita, naamini ilikuwa hivyo, Jumapili iliyopita asubuhi, kama *Mfalme Aliyekataliwa*. Kuna mtu yeyote aliyeipata kanda hiyo hivi sasa? Nafikiri wanazo, nanyi mnaweza kuzipata mkizitaka, *Mfalme Aliyekataliwa*.

10 Sasa ni siku chache tu na tutaanzia kule … huko Middletown, Ohio. Tunataka wote waliopanga likizo za—zao kwenye wakati huo wahakikishe kukutana nasi kule, maana tunatarajia wakati mzuri wa ushirika huko Middletown, Ohio. Daktari Sullivan ndiye mwenyekiti, nafikiri, wa hiyo kamati. Na utakuwa wa usiku kwa siku tano, nitakuwa nikihubiri kama m—mgeni kwenye Mkutano wa Kimataifa wa kanisa la Mchanganyiko wa Madhehebu. Na halafu—halafu baada ya huo, tutakuwa na mkutano wetu wenyewe tangu wakati huo na kuendelea. Tayari tumeipanga hata tarehe kumi na mbili, lakini kwa uelewano kwamba huenda tukaendelea hata kwa wiki nyingine moja baadaye, inategemea tu jinsi Roho Mtakatifu anavyoongoza. Sote tunataka kuongozwa na Roho; lile tu Roho analosema fanya, basi tunalifanya haraka.

11 Na hebu na tukumbuke wakati tunapomtii Roho, somo moja kuu tunalotaka kujifunza, kamwe si la haraka. Unaona, chukua wakati wako, uwe na imani. Kama tumemwomba Mungu jambo lo lote, kumbukeni Mungu hujibu maombi. Yeye huyajibu katika wakati Wake, jinsi lilivyo bora zaidi, analifanya litende kazi vizuri tu kwa ajili yetu. Na kama hivyo sivyo, basi tunafanya nini hapa asubuhi ya leo? Tuna—tunadai Ukristo kwa ajili gani? Mungu … Kama hili si Neno la Mungu, basi si la kweli, basi tunajikuta tu watu wenye huzuni kuliko watu wote.

Nina furaha sana kuiunganisha mioyo na wengi hapa wanaojua kwamba Hili ni Neno la Mungu lisilokosea. Basi Hilo, Hilo ni Kweli kwa kila Neno, kila Neno Lake, kila fungu Lake. Na kwa neema ya Mungu,nimejaliwa kuiona ile Nchi ambayo siku moja tutaizuru.

12 Jana. Watu hawajui jinsi nyakati za huzuni huandamana na huduma ya aina hii. Nilishuka moyo sana, nami nikamwambia mke wangu, "Laiti ningaliaga dunia."

Akasema, "Kwa nini unasema hivyo, Bill?"

Nikasema, "Loo, hapa nina shida na kadhalika."

Na ndipo ilionekana kama kwamba Roho Mtakatifu alisema, "Je! Unajaribu kuziepa? Je! wewe, unajaribu kuzipiga chenga?" Unaona?

"La," nikasema, "hebu nisimame moja kwa moja mbele za hayo yote na kuyakabili. Unaona, ninii tu …" Unaona?

Ni bora zaidi. Kwa kweli, hakika, nasema jambo hili kwa ushahidi wa kuona kwa macho, ya kwamba mara baada tu ya maisha haya kwisha, tunaingia katika Nchi ambayo imepita chochote ambacho mtu yeyote angeweza kuwazia. Na kama kuna wageni wo wote hapa, natumaini ya kwamba hamninii … Naomba kwa Mungu kwamba hamtanichukulia kama mshupavu wa dini. Na—nataka, kama kuna jambo lolote, niwe mwaminifu na kusema Kweli. Na ingenifaa nini kwangu kusema jambo fulani ambalo lilikuwa ni kosa, wakati kuna ninii—kuna mengi sana hapa yaliyo Kweli? Sisi, kwa nini tuseme jambo lolote la makosa juu yake? Unaona? Hilo, Hilo ni Kweli tu.

13 Na, si ajabu, naamini Paulo alinyakuliwa juu katika mbingu ya tatu, naye aliona mambo ambayo hakuweza kutamka. Na siku moja akasema, "Mambo ambayo jicho halikuyaona, wala sikio haliyasikia,wala hayakuingia moyoni mwa mwanadamu, yale mambo ambayo Mungu aliwaandalia (aliwawekea) hao wampendao Yeye."

Loo, tunaishi tu … Tunaishi katika lundo la takataka chini hapa, hivyo tu, lundo tu la takataka lililojaa-moshi unaofuka kutoka kwenye kinyaa. Wa … Hata kama sisi wenyewe hatukuchafuliwa na hayo, tunaishi ndani yake, mahali ambapo moshi unafuka kutoka kwenye miali ya moshi wa dhambi. Moja ya mambo ya kuchukiza sana ninayoweza kuwazia, ni jalala la kale la jiji linaloteketea kwa moto. Ulipata kuwa karibu na moja? Hiyo harufu ya kutisha, iliyochafuliwa ya moshi ikitokea katika kila aina ya uchafu. Na—na unaivuta, na inakuchefua tu.

14 Nakumbuka iliponibidi kushuka kwenda New Albany, huko chini ya … chini ya Barabara ya Kumi na Nane, kule mahali ambapo jalala la takataka la kale lilipokuwa, nami inanibidi kuchukua kule chini na kusoma mita. Nami niliichukua tu siku hiyo ilipofika, njia ya kumi na nane, wakati iliponibidi kuipitia hiyo chini kule, kwa sababu ilikuwa ni kunusa hiyo harufu ya kuchukiza sana. Na hata hivyo, miili ya panya na mbwa na kila kitu ilikuwa kule, mwajua, hiyo ilikuwa ikiteketea na huo moshi wa kale ukifuka kutokea

humo.

Sasa, hata hivyo, hivyo ndivyo maisha haya yanavyolinganishwa nalo, yakiwa katika ubora wake kabisa. Yanaugua tu, dhambi inanuka kutokea kila mahali, jinsi hilo lilivyo, tukinena kiroho. Lakini, loo, mahali ambapo upepo unavuma wazi, na kila kitu ni cha kupendeza na amani na furaha na Uzima wa Milele, ng'ambo tu ya ule mto. Lakini sisi tuko vitani, kwa hiyo hebu tusilale tu na kusema "hebu na tuharakishe tufike kule," hebu na tumlete kila mtu ambaye tunaweza kumleta. Ndiyo.

15 Na sasa kusudi la masomo haya ni kuwatia nanga wale ambao tayari wamevuka na kufika Nchini. Kusudi la somo hili, kule kujifunza Kitabu hiki cha Waefeso, ni kuliweka kanisa mahali pake ambapo linasimama imara katika Kristo. Ni mfano wa Agano la Kale na Kitabu cha Yoshua, ambapo Yoshua aliwagawia. Jumapili iliyopita tulikuwa nalo, ambapo Yoshua aliigawa ile ardhi kwa kila mtu. Naye alifanya hilo kwa uvuvio.

Jinsi Musa alivyo … alivyowatoa watu kutoka Misri, vitunguu saumu, vitunguu, wakatoka, naye akawapa mahali ambapo Mungu alikuwa ameahidi miaka mia nne baadaye … ama miaka mia nne hapo kabla, kwamba Yeye angewaleta mahali fulani, nchi nzuri yenye wingi wa maziwa na asali. Naye Musa akawaongoza wana wa Israeli moja kwa moja hadi kwenye nchi ile, lakini yeye hakuwaingiza.

Na Yesu, kwa watu wa kiroho, kwa watu ambao wataninii … tumeahidiwa Roho Mtakatifu tangu hapo mwanzo, Yesu alituongoza kwenye ile ahadi. Lakini Roho Mtakatifu akaja, kama Yoshua, kutwaa mamlaka na kuongoza na kutuelekeza mpaka kuja na kuimiliki nchi, ama kumiliki kanisa. Tunaona, kimsingi, basi, ya kwamba katika ninii yetu …

16 Sasa hapa ndipo ambapo, labda, watu wanaweza kufikiri ya kwamba mimi ni mjeuri na ninajaribu kutowajali ndugu. Mimi siko hivyo! Mungu na awe Hakimu wangu, sivyo nilivyo. Unaona? Ninajaribu tu kuonyesha jambo ambalo ni Kweli. Unaona? Tumechagua viongozi, waliochaguliwa na wanadamu, badala ya kuongoza, viongozi, uongozi wa Roho Mtakatifu. Tumewataka wanadamu watugawie sehemu yetu na kutuongoza, madhehebu kama Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheran, Church of Christ, Pentekoste, na madhehebu mbalimbali, kuweka madhehebu kama mfano, nasi tunaufuata huo. Lakini sisi ni …

Hakuna mahali popote katika Biblia ambapo tunapaswa kufanya mambo kama hayo. Hakuna hata fungu moja la Maandiko, katika Biblia yote ya Mungu, ambapo Yeye aliwahi kufanya kanisa dhehebu ama mahali ambapo aliwahi kunena juu ya dhehebu, hakuna mahali hata pamoja katika Biblia. Lakini daima ni kinyume chake. Yeye hataki tufananishwe kama mambo ya ulimwengu. Yeye anatutaka sisi tuwe wa kipekee, waliotengwa.

Simaanishi sasa kuwa "wapumbavu," kama tunavyosema. Namaanisha tuwe watu walioitwa wakatoka, loo, taifa takatifu lililobarikiwa, tukiishi maisha ambayo hayana shutuma, tukitenda, tukienenda kama tu Yeye angelienenda, akifanya kazi ndani yetu, kwa kuwa sisi tu kazi Yake, tulioumbwa katika Kristo Yesu kwa matendo mema.

17 Sasa, Jumatano usiku, wengi wenu hamkuwa hapa Jumatano usiku, bali tuliingia katika … Naamini ni aya ya 3 ama ninii … La, ni aya ya 5.

> … *Ili tufanywe wanawe,* au watu kuwekwa mahali pao …

Jinsi ambavyo Mungu, akijaribu kuwaweka watu Wake. Na wakati Mungu anapomweka mtu mahali pake, ndipo, loo, kanisa lote linataka kuwa kama huyo, wapate vitu vya aina ile ile, wafanye mambo yale yale. Sisi tumeumbwa tofauti, tumetengenezwa tofauti, tumepewa malezi tofauti, nasi tumewekwa mahali petu tofauti, kila mmoja kwa ajili ya kazi tofauti; labda mmoja kwa ajili ya kazi fulani ndogo tu, mwingine kwa ajili ya kazi kubwa. Ninaamini ilikuwa ni Daudi ama mmoja wa manabii, nasahau sasa, kasema, "Ni bora niwe zulia la mlangoni wa mlango kwenye Nyumba ya Bwana, kuliko kuwa … kukaa katika mahema pamoja na wao- … waovu."

18 Sasa tutasimama kwa sekunde moja tu juu ya kufanywa wana wenye mamlaka, aya ya 5, tukijaribu kuendelea kusoma umbali tuwezao juu yake. Lakini sasa kumbukeni lile somo, kwa jumla ni juu ya kuwekwa mahali pako. Ni wangapi wanaofahamu jambo hilo? Hebu tuwasikie mkisema hilo kwa neno moja. Kuweka [Kusanyiko linasema, "Kuweka" — Mh.] Mwili ["Mwili"] wa Yesu Kristo ["wa Yesu Kristo"] mahali pake ["mahali pake"] katika Kristo ["katika Kristo"] ambapo Roho Mtakatifu ["ambapo Roho Mtakatifu"] anatuongoza ["anatuongoza."]. Haya basi, sasa tumelipata, unaona. Kutuweka mahali petu, Kitabu cha Efeso kitafanya hivyo.

19 Na mwangalie huyu mwalimu hodari, Paulo. Jambo la kwanza analofanya ni kuondolea mbali wazo lote la kuanguka. Kuondolea mbali wazo lote la kila mara "kuwa Mkristo leo na kesho nimepotea, na kesho yake Mungu alinihukumu na siku inayofuata nimerudi tena." Huo ni upuuzi! Sasa hiki ni … Kitabu hiki hakielekezwi kwenye mafundisho ya kiinjilisti, mahubiri ya wainjilisti. Sisi hatuninii … Sigusii jambo hili huko viwanjani. Nalileta hili kanisani, kwa kuwa Paulo aliliandikia watakatifu, wale walioitwa na kuhifadhiwa, na wamejazwa na kuwekwa kando, na wako katika Roho Mtakatifu, tayari wako katika Nchi ya Kanaani.

Yeye anajaribu kuwaambia, jambo la kwanza, sahauni kabisa kwamba mtapotea na mtafanya *hivi*, na mnaogopa *hili*. Msiogope chochote, kwa kuwa anajaribu kuwaambieni mlipo, ninyi ni akina nani, jinsi mnavyosimama.

20 Sasa, huenda ukakosea, na kila unapofanya kosa lo lote utalilipia. Naam, bwana, utavuna unachopanda! Lakini hilo halina uhusiano wo wote na wokovu wako. Unapozaliwa kwa Roho wa Mungu, una Uzima wa Milele na huwezi kufa tena kama Mungu asivyoweza kufa. Wewe ni sehemu ya Mungu, wewe ni mwana wa Mungu.

Nilizaliwa Branham. Huenda ukanitengenezea jina lingine, baadhi ya majina mengine, lakini hutanifanya nisiwe hata kidogo, mimi bado ningali Branham. Nilizaliwa Branham, daima nitakuwa Branham. Nita- … Huenda nikaharibiwa sura sana siku moja, niambukizwe yabisi kavu, nipate ajali ya gari na nijeruhiwe sana hata nionekane kama mnyama, lakini bado nitakuwa Branham! Kwa nini? Damu ya Branham iko ndani.

21 Hivyo ndivyo wewe ulivyo. Na mradi tu Mungu amekufanya … Sasa kumbukeni, siwazungumzii hao walio nje ya Kristo. Nawazungumzia hao walio ndani ya Kristo. Unaingiaje katika Kristo? "Kwa Roho mmoja!" Herufi kubwa R-o-h- … ambayo inamaanisha, "Kwa Roho Mtakatifu mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Je, sisi … Sisi tunaingiaje? Kwa ubatizo wa maji? Jinsi nisivyokubaliana na ninyi Wabaptisti na ninyi Kanisa la Kristo. Si kwa ubatizo wa maji, la hasha! Wakorintho wa Kwanza 12, ilisema, "Kwa Roho mmoja, Roho Mtakatifu, tunaingizwa katika Mwili huo." Nasi tunakuwa salama tu kama vile Mwili huo ulivyo salama. Mungu ni … aliahidi jambo hilo.

22 Mungu angewezaje kumhukumu tena, na huku Yeye alienda Kalvari? Akipanda kwenda Golgotha, alipigwa, akajeruhiwa, Yeye asingeweza kuponya, hata hangeweza kunena neno, ilikuwa vigumu. Kwa sababu gani? Yeye alikuwa amebeba dhambi za ulimwengu juu Yake. Si kwa sababu Yeye alikuwa mwenye dhambi, bali "Yeye alifanyika dhambi" kwa ajili yangu na kwa ajili yako. Dhambi zote za ulimwengu tangu Adamu mpaka kuja Kwake, zilikuwa juu ya bega Lake. Na Mungu hakuwa anamwadhibu Mwanawe. Alikuwa akiadhibu dhambi. Mnaona jinsi lilivyokuwa la kutisha? Alikuwa akifanya upatanisho. Alikuwa akitengeneza njia ya kuepukia kwa wale wote ambao Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alijua wangekuja. Tutaingilia jambo hilo katika dakika chache.

23 Sasa, basi, unapokuwa "kwa Roho mmoja tumebatizwa katika Mwili huo, Mwili mmoja, ambao ni Kristo," nasi tuko salama milele.

Sasa, hapo ndipo linapoonekana kama linagusa sana, hasa hao—hao—waumini Waarmenia, ya kwamba wao … inawabidi kufanya jambo fulani kusudi wastahili, ama jambo fulani la kustahilisha. Inawezaje kuwa kwa mambo mawili kwa wakati ule ule? Aidha ni kwa neema ama kwa matendo, mojawapo. Haiwezi kuwa kwa jambo lile lile, ni kwa mambo mawili tofauti; haina budi kuwa ni kwa njia moja. Ni …

24 Mimi, jamani, siwezi kuona kitu kingine ila neema ya Mungu. Nimeumbwa hivyo. Daima nimeamini katika neema. Mimi ni neema tu kila mahali, hivyo tu. Si mimi—mimi … hata maishani mwangu, nilipokuwa mvulana, nikuweza kuona chochote, neema tu, neema. Wao wanasema, "Ni—nita- … Ukikuna mgongo wangu nami nitakuna wako." Vema, huo ni msemo wa kutisha. Lakini sijali kama utaukuna wangu au la, kama wako unahitaji kukunwa, nitakukuna hata hivyo. Unaona, neema. Naam, bwana. Unaona, neema hutenda kazi kwa upendo. Kama unahitajihilo! Haidhuru kama hukufanya kitu cho chote kamwe, si—sina uhusiano wo wote nawe, kama ukihitaji nitalifanya hilo hata hivyo. Neema! Kwa sababu unaihitaji!

25 Nilihitaji kuokolewa. Hakukuwa na kitu kingeweza kuniokoa. Hakuna kitu ningeweza kufanya juu yangu mwenyewe, singeweza kujiokoa hata nifanyeje. Lakini nilihitaji kuokolewa, kwa sababu niliamini katika Mungu fulani. Naye Mungu akamtuma Mwanawe, aliyefanywa katika mfano wa mwili wenye dhambi, apate kuteseka mahali pangu, nami nikaokolewa, kwa neema pekee niliokolewa. Singeweza kufanya hata jambo moja, ama wewe ufanyae kujiokoa mwenyewe. Na wale aliotangulia kuwajua tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu …

26 Tumekuwa nalo, Jumatano iliyopita. Tulimwona Mungu katika Elah Yake, Elohim, na tukaonyesha kwamba Yeye alikuwa anayeishi peke Yake. Lakini ndani Yake kulikuwa na Ubaba, ndani Yake kulikuwa na sifa mbalimbali, kama vile Mwokozi, kama vile Mponyaji. Hizo zote zilikuwa ndani ya Mungu, na Mungu alikuwa akikaa peke Yake. Lakini kwa kuwa Yeye alikuwa Mwokozi, Yeye alikuwa Ba… Yeye hakuwa na Malaika, hakuwa na kitu chochote. Hakukuwa na kitu chochote ila Yeye Mwenyewe. Yeye alikuwa akikaa peke Yake. Hakuna kitu kingine kilichokuwepo ila Mungu.

Lakini kwa kuwa Yeye alikuwa Mungu, basi hapana budi kuwe na kitu cha kumwabudu, kwa sababu Yeye alipenda kuabudiwa. Na Aliye Hai akaumba viumbe wapate kumwabudu Yeye. Sasa, kwa muda mfupi, hebu na tuliguse tena, kwa muda mfupi sasa, hatutapitia kwenye jambo hilo lote, bali mtalipata kwenye kanda. Lakini basi kwa sababu Yeye alikuwa Mungu, aliwafanya Malaika, na Malaika wakamwabudu. Malaika wangali wanamwabudu. Mbona, Malaika wanaosimama Mbele za Mungu wana

sita, jozi za mabawa, mabawa sita. Kwa mawili wanafunika nyuso zao, mawili juu ya miguu Yao, na wanaruka kwa mbili, katika Uwepo Wake, wakilia mchana na usiku, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyenzi." Hivyo ndivyo yasemavyo Maandiko. Wao walimwabudu, sasa Yule aliumba kitu fulani cha kumwabudu Yeye.

27 Kisha ndani Yake mlikuwemo sifa ya kuwa Mwokozi. Mmoja wa hao Viumbe angewezaje, wakati hakukuwemo na dhambi wala mawazo ya dhambi, mmoja wao angewezaje kupotea? Isingewezekana. Kwa hiyo ilibidi kuwe na kitu fulani kilichofanywa ambacho kingeweza kupotea, ili kwamba aweze kuwa Mwokozi. Ndani Yake kulikuwa na Mponyaji. Mnaamini Yeye ni Mwokozi? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnaamini Yeye ni Mponyaji? ["Amina."] Lakini vipi kama hakungekuwako na kitu cha kuokoa au kuponya? Unaona, ilibidi kuwe na kitu kilichofanywa namna hiyo.

Kwa hiyo sasa, Yeye hakulifanya hivyo, bali alimpa mwanadamu uhuru wa kuamua takalo, "Kama ukichukua *hii* utaishi, kama ukichukua *ile* unakufa." Na kila mtu anayekuja ulimwenguni angali amewekwa katika hali ile ile. Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alijua ni nani angefanya na ni nani asingefanya. Kama Mungu akiwa …

28 Swali liliulizwa jana na mwanatheolojia, kwangu mimi, ambaye amekuwa akihudhuria mikutano hii ama akisikiliza kanda, kasema, "Swali moja!" Yeye alisema, "Basi Mungu yuko kila mahali? Halafu," akasema,"Yeye anaweza kuwa kila mahali?"

Nikasema, "Yeye hayuko kila mahali kwa jinsi neno linavyozungumzia kuwa kila mahali. Yeye hawezi kuwa Aliye Hai halafu na awe kila mahali. Kama Yeye yuko kila mahali, kwa nini uombe kwa ajili ya Roho Mtakatifu? Kama Yeye yuko kila mahali, Yeye amejaza kila mwanya, kona, ufa, kila seli, nyuzi, kila kitu kingine kilichopo." Nikasema, "Kwa nini alimtafuta Musa, kama Yeye yuko kila mahali, mwishoni? Kwa nini Yeye alikimbia huku na huko kwenye bustani ya Edeni, akipiga kelele, 'Adamu, Adamu, uko wapi?' Kama Yeye yuko kila mahali?"

Yeye yuko kila mahali kwa sababu Yeye anajua yote. Yeye anajua kila kitu kwa sababu Yeye hana ukomo, na kutokuwa na ukomo kunamfanya Yeye awe kila mahali. Akiwa kila mahali, halafu, akiwa hana kikomo, ndipo, Yeye huketi katika Mbingu. Yeye anakaa mahali fulani kwa sababu Yeye ni Aliye Hai.

29 Lakini, akiwa asiye na ukomo, basi Yeye anajua mambo yote. Akijua kila wakati mbu anapopepesa jicho lake. Anajua kila nyuki, anakoenda kwenye sega kupata asali yake. Yeye anajua kila shomoro anayekaa kwenye mti. Yeye anajua kila wazo lililo moyoni mwako, kwa sababu Yeye hana ukomo na anajua yote. Hiyo ni kusema, Yeye si tu kwamba hana ukomo tu, Yeye anajua yote, Yeye anajua kila kitu. Lakini Yeye ni Aliye Hai, Mungu ni Aliye Hai, na kutoka kwa Aliye hai huyu haya yakaanza kutokea.

30 Na dhambi, nilisema hivi majuzi usiku, dhambi si kitu kilichoumbwa. Hakuna kilichoumbwa ila ukamilifu. Mungu aliumba vitu vyote vizuri. Dhambi si kitu kilichoumbwa. Kasema, "Vema, huo ni uumbaji wa dhambi hasa." Mmesikia hilo. Lakini hilo ni kosa. Dhambi … Kuna Muumba mmoja tu, huyo ni Mungu. Mungu asingeweza kuumba dhambi, kwa sababu Yeye ni mtakatifu na hakuna kitu ndani Yake cha kuifanya. Dhambi ni upotovu; si kitu kilichoumbwa, bali ni upotovu. Uzinzi ni tendo la haki lililopotoshwa. Uongo ni ukweli uliosemwa vibaya. Dhambi yoyote, dhambi yoyote ni haki iliyopotoshwa.

31 Kwa hiyo sasa, Mungu huweka. Yeye tayari amejidhihirisha Mwenyewe, Yeye ni Mungu. Yeye tayari amejidhihirisha Mwenyewe kama Mwokozi, mwanadamu alipotea Naye akamwokoa. Yeye tayari amejidhihirisha Mwenyewe kama Mponyaji. Haidhuru watu wanasema Yeye ni nani; Naye ndivyo alivyo, hata hivyo, vile vile. Yeye ni Mponyaji, Yeye ni Mwokozi, Yeye ni Mungu, Yeye ni wa Milele. Naye ana kusudi. Na kusudi Lake lilikuwa, hapo mwanzo, kuwaumba viumbe ambao wangempenda na kumwabudu.

Naye akaumba viumbe, na viumbe vikaanguka. Na kisha Mungu, kwa kutokuwa Kwake na ukomo, aliangalia kupitia mlolongo wa wakati akaona kila mtu ambaye angeokolewa. Kila mtu, Yeye alijua hilo kwa kutangulia … kwa kujua tangu zamani. Kwa hiyo kama Yeye, kwa kujua tangu zamani, alijua ni nani angeokolewa na ni nani hangeokolewa, Yeye angeweza kuchagua tangu zamani. Kwa hiyo, hilo neno hilo si neno baya hata hivyo, sivyo? Yeye angeliweza kuchagua tangu zamani, kwa sababu alijua ni nani angeokoka na ni nani asingeokoka. Kwa hiyo, kusudi apate kuwapata wale ambao wangeokoka, ilimbidi kufanya u—upatanisho kwa ajili ya dhambi zao. Loo, kama tunaweza, tunataka kulifikia jambo hilo, aya chache tu hapa chini. Yeye alitangulia kutuchagua tangu zamani tupate Uzima wa Milele, akijua kwamba wale ambao wangeweka kando kila kitu, na hata ionekane ni gumu vipi kwa watoto wa ulimwengu, haingemaanisha lolote kwao, kwa sababu wao walikuwa watoto wa Mungu. Naye aliwaita.

32 Naye alimtuma Yesu, ili kwamba Damu Yake ipate kuwa upatanisho, Upatanisho wa Damu, kufanya upatanisho, ama ku—kukubalika, ama utakaso. Utaratibu wa kutakasa ili daima … Si wakati mmoja tu kwenye uamsho mmoja, bali "yu hai daima, akiwaombea," hivi kwamba Mkristo anawekwa msafi mchana na usiku. Hiyo hapo Damu ya Yesu Kristo inayofanya ku—kukubalika msalabani pale, kwenye … katika Uwepo wa Mungu, ambayo hutusafisha daima, mchana na usiku, mbali na dhambi zote. Nasi tumeingizwa ndani salama. Kuingizwa ndani vipi? Na Roho Mtakatifu, katika Mwili wa Bwana Yesu, na tuko salama.

"Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenituma, yuna Uzima wa Milele na hataingia hukumuni kamwe, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hakuna hukumu tena! Mkristo kamwe haingii hukumuni. Kristo alikwenda kwa ajili yake. Wakili wangu alisimama mahali pangu. Yeye alinitetea, ya kwamba sikujua. Yeye alimwambia Baba kwamba sikustahili, ya kwamba sikujua kitu. Lakini Yeye alinipenda na akachukua mahali pangu, na akanitetea, na leo niko huru! Naam, bwana. Naye akamwaga Damu Yake, kuitoa paleo kwa ajili ya dhambi zetu.

33 Mnakumbuka Jumatano iliyopita usiku, hapana Mkristo … Mkristo hutenda dhambi, bali mwenye dhambi hawezi kutenda dhambi. Mwenye dhambi hatendi dhambi, kwa sababu yeye ni mwenye dhambi. Kwanza yeye ni mwenye dhambi tu, na hivyo tu. Hapa, chukua u—upande wa nyuma wa kitabu hiki, ni nyeusi, ni sehemu gani iliyo nyeusi? Chote ni cheusi. Hakuna weupe kwenye hicho, ni cheusi. Unasema, "Sehemu *hii* hapa." La, sivyo, kitu hicho chote ni cheusi. Chote ni cheusi. Hivyo ndivyo alivyo mwenye dhambi. Kwanza yeye amehukumiwa. Vema, unasema, "Vipi kama akifanya uzinzi? Vipi kama akimnajisi mwanamke fulani? Vipi kama a—vipi kama anacheza kamari? Vipi kama akimpiga mtu fulani risasi?" Hiyo si kazi yetu. Hiyo si kazi yetu, tuna sheria hapa chini kushughulikia jambo hilo. Sisi si watengenezaji, sisi ni wahubiri wa Injili. Hatumhukumu kwa yale aliyofanya, hatumhukumu kwa kufanya uasherati. Tunamhukumu kwa sababu yeye ni mwenye dhambi! Kama yeye ni Mkristo, asingefanya hivyo. Hiyo ni kweli. Kama amebadilishwa, hatafanya hivyo. Lakini kwa sababu yeye ni mwenye dhambi, hilo ndilo linalomfanya afanye hivyo.

34 Hapo ndipo linapobomoa m—mhimili chini ya washika sheria. Naam, bwana. Ndugu, hebu nikwambie, "Si kwa matendo, bali kwa neema tumeokolewa, na hiyo ni kwa imani." Naam, bwana. Sasa, sitawalaumu ndugu washika sheria, wao ni ndugu zangu. Nao watakuwako kule kama tu vile hao wengine watakavyokuwa kule, kwa maana Mungu alichagua tangu zawani Kanisa Lake liwe kule. Lakini jambo ni kwamba, mna—mnawatia watu wasiwasi sana, hivi hawajui nini. "Leo, vema, labda kama mimi—mimi …" Hebu wajue tu; mradi tu wana njaa ya ulimwengu, kwanza hata hawako kule.

35 Mimi siishi mwaminifu kwa mke wangu kwa sababu nafikiri angenitaliki. Ninaishi mwaminifu kwa mke wangu kwa sababu ninampenda. Tumechukua msimamo halali, kwamba tunapendana sisi kwa sisi. Kwanza, kabla ya kuweko, ilibidi upendo uwepo. Ninampenda. Ingawa ninaamini kama nilifanya kosa fulani, yeye angenisamehe, hata hivyo nisingelifanya jambo hilo hata hivyo. Nampenda.

Hivyo ndivyo ilivyo na Kristo. Kama ni—kama nikiishi … Mimi nina umri wa miaka hamsini, kama nikiishi kuwa na miaka tisini ama mia moja, niwe na miaka mingine hamsini ya kuhubiri; nami nisihubiri hata mara moja, nishuke niende nikakae mtoni, nimeokolewa hata hivyo. Mungu aliniokoa kwa neema Yake, nisivyostahili kwa lolote ningaliweza kufanya, niliyofanya, ama kitu cho chote kile. Ninahubiri kwa sababu ninampenda Yeye na ninawapenda watu Wake. Na hiyo ndiyo sababu najua nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa sababu kwamba nawapenda na ninaenda kuwatafuta. Haidhuru wako katika hali ya namna gani, naenda kuwatafuta hata hivyo. Naenda kuwatafuta haidhuru, niwavute hata hivyo. Kama wahudumu hawakubaliani na wengine hawakubaliani, na madhehebu hayakubaliani, hilo halinizuii. Kuna jambo fulani! Hilo halikumzuia Yeye! Yeye alikuja moja kwa moja katikati ya kutokuamini, na hilo halikumzuia, Yeye alisonga mbele moja kwa moja hata hivyo. Hivyo ndivyo tunavyofanya, tunaenda kuwatafuta, kuwapata kwa vyovyote. Haidhuru, waendee, wanyakue, washikilie kwa nguvu zako zote. Hujui hao ni akina nani. Waokoe. Hiyo ni kwa sababu ya upendo. Si ati kwa sababu "inanipasa kufanya hivyo," bali ni kwa sababu napenda, kwa sababu unapenda.

36 Wakasema, "Inanipasa kwenda nikasahihishe jambo hilo na mwanamke huyo, lakini, nakwaambia sasa hivi, nadhani kwa sababu mimi huenda kanisani ninapaswa kwenda kulisahihisha." La, wewe ndiwe unayepaswa kujiweka sawa, kwanza. Unaona? Unaona? Kama huna upendo wa Mungu moyoni mwako, kitu fulani kingine kinakufanya ujue kwamba umekosea, basi unaenda—ndipo unaenda kulisahihisha mbele za Mungu. Ndipo utalisahihisha kwa jirani yako.

Yesu alifundisha jambo lile lile. Yeye alisema, "Kama ukija madhabahuni, na kuna ninii … ukumbuke kuna jambo dhidi ya jirani ama ndugu, nenda ukarekebishe kwake, kwanza."

37 Sasa, sasa katika nyakati ambazo hazina budi kuja. Tulikuwa nayo Jumatano usiku, "madhihirisho." Tunalipata tena asubuhi ya leo, katika "madhihirisho ya wana wa Mungu." Kwa maneno mengine, Mungu anangojea. Na kisha kwenye mwisho wa wakati ambapo sisi sote tutasimama mbele Zake. Malaika hawakupotea. Hawatajua jinsi ya kufurahia hizo baraka kama tujuavyo, hao kamwe hawakupotea. Lakini mimi najua nilikotoka, najua ule mwamba nilimotolewa, mwenye dhambi. Unajua ulikotolewa. Sasa tukiishapatikana, basi tunaweza kusimama mbele za Mungu. Loo, hiyo itakuwa ni siku ya jinsi gani!

38 Kisha kufanywa wana wenye mamlaka, kuwekwa mahali petu. Sasa, wema wa Mungu unapaswa kutenda kazi. Na sasa kama ninaweza kuwaeleza jambo hili, basi tutaanza sasa hivi ile aya ya 5, nataka kuisoma.

> *Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake* Mwenyewe.

Mungu hupendezwa kufanya mapenzi Yake, kufanya wana wenye mamlaka, kuwaweka mahali pao. Sasa Yeye anafanya nini? Akiliweka Kanisa Lake mahali pake. Kwanza, Yeye ameliita kanisa Lake, Methodisti, Presbiteri, Lutherani, Baptisti, akiwaita. Kisha Yeye alifanya nini? Akamtuma Roho Mtakatifu na kuwapa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

39 Nawatakeni ninyi Wapentekoste mwondoe jambo hili mioyoni mwenu. Pentekoste si dhehebu; Pentekoste ni tukio. Ni Roho Mtakatifu. Si shirika la dini. Usingeweza kumfanya Roho Mtakatifu dhehebu. Yeye hatavumilia jambo hilo. Sasa mna dhehebu mnaloliita hivyo, bali Roho Mtakatifu hutoka nje kabisa na kuwaacha mmeketi papo hapo mlipo, na anazidi tu kusonga mbele. Unaona? Pentekoste si dhehebu; Pentekoste ni tukio.

40 Na ndipo Mungu akawapa watoto Wake Kuzaliwa upya, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Waliukaribia sana walipojisafisha, kupitia Nazarayo, Pilgrim Holiness. Ndipo wakaingia kwenye ule ujuzi wa pentekoste, ama ubatizo wa Roho Mtakatifu, kurejeshwa kwa karama. Waliondoka wakaenda wakinena kwa lugha na kufasiri lugha, na wakapewa karama za uponyaji na miujiza, na ishara na maajabu vikianza kuambatana nao. Sasa wao ni watoto, wao ni watoto wa Mungu. Wao wako mahali pao katika Kristo. Wanakuwa watoto kwa Kuzaliwa. Na Kuzaliwa upya na kuongoka Kwenyewe ni Roho Mtakatifu.

Hata hujaongoka mpaka umepata Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema. Yesu alimwambia Petro, mwulize mtu ye yote, soma Maandiko yako, yeye alihesabiwa haki kwa kumwamini Bwana Yesu, akawa mfuasi, mtume. Yesu alimpa funguo za ule Ufalme. Na Yohana 17:17, Yeye aliwatakasa, akawapa nguvu, akawatuma, wakatoa pepo na kadhalika, akawatakasa. "Uwatakase, Baba, kwa Kweli Yako. Neno Lako ndiyo Kweli. Ninajitakasa Mimi Mwenyewe kwa ajili yao."

41 Hayo ni baadhi ya maneno matamu sana niliyopata kusikia. "Baba, najitakasa Mimi Mwenyewe kwa ajili yao." Je, mnajua Yeye alikuwa na haki ya kuwa na nyumba? Yeye alikuwa mwanadamu. Unajua ni kwa nini alikuwa na haki ya kuwa na mke? Yeye alikuwa Mwanamume. Yeye alikuwa na haki ya mambo haya yote, lakini Yeye akasema, "Baba, najitakasa Mimi Mwenyewe kwa ajili yao. Najitakasa Mimi Mwenyewe."

42 Nilizungumza na maskini mhubiri mmoja jana, nitaenda kumsaidia kuhubiri katika siku chache usiku hapa kwenye barabara kuu. Nami nilimwuliza juu ya jambo fulani, akasema, "Naam, Ndugu Branham, lakini wengi wa watu wangu hawaamini jambo hilo."

Nikasema, "Karibu wote ni washika sheria?"

"Naam." Ndugu huyo haamini jambo hilo. "Lakini," akasema, "kwa ajili yao!" Loo, nilitaka kukumbatia shingo yake. "Kwa ajili yao, unaona, najitakasa mimi mwenyewe kwa ajili yao."

43 Loo, Yesu alikuwa akiwafundisha watu kumi na wawili, ili kwamba kupitia kwa hao watu kumi na wawili apate kuipeleka Injili ulimwenguni. Naye akasema, "Kwa ajili yao najitakasa Mimi Mwenyewe." Jifanye mwenyewe kwa ajili ya jirani yako, kwa ajili ya mtu mwingine. "Usitumie uhuru wako kwa kusitiri mambo," alisema Paulo, "bali wewe mwenyewe jitakase!" Enenda katika tabia njema kwa jirani yako, kama vile Mkristo halisi anavyopaswa kufanya. Hebu mazungumza yako yawe, kama ukikutana na adui yako, jitakase wewe mwenyewe kwa ajili yake, bila kujua jambo ambalo ungefanya.

44 Sasa kumweka mwana mahali pake. Jambo la kwanza baada ya mwana kuingia, akawa mwana, lakini basi tunaona tabia yake ndiyo iliyomfanya afanywe mwana mwenye mamlaka, kama alikuwa na tabia nzuri au la.

Na ni—ni kipentekoste … Sasa hebu niwaonyeshe tu kwamba Pentekoste si dhehebu. Ni Wabatisti wangapi humu ndani waliokuwa Wabatisti, waliompokea Roho Mtakatifu, hebu tuone mikono yenu. Unaona? Ni Wamethodisti wangapi walio humu ndani waliompokea Roho Mtakatifu, inueni mikono yenu. Ni Wanazarayo wangapi humu ndani waliompokea Roho Mtakatifu, inueni mikono yenu. Mpresbiteri, mmempokea Roho Mtakatifu? Unaona? Mluteri? Madhehebu mengine, ambayo hayakuwa ya Pentekoste kabisa, yalikuwa tu ya dhehebu fulani, yaliyompokea Roho Mtakatifu, hebu tuone mkono wako. Unaona? Kwa hiyo basi Pentekoste si dhehebu, ni ujuzi.

45 Sasa, Mungu alikuingiza katika Mwili wa Kristo. Sasa Yeye anafanya nini? Baada ya kujithibitisha mwenyewe, ukajitakasa mwenyewe kwa tabia yako njema, mtiifu kwa Roho Mtakatifu, haidhuru ulimwengu ulisema nini.

46 Ni—nitasisitiza jambo hili sana, unaona, kwa sababu … Simaanishi kuwa mkatili. Mimi—mimi … tafadhali msi—msi—kweli msifikiri hivyo, mnaona. Msifikiri kuwa mimi-mimi kweli ni mkatili. Si—sitaki kuwa hivyo. Kile kinachonichosha, ni kuwachukua watu na kuwahubiria Kweli hii iliyotumwa na Mungu, nao watageuka moja kwa moja na kuendelea kufanya jambo lile lile, na kusema wana Roho Mtakatifu. Hilo karibu linakuangamiza, unaona. Kuna nini? Wanarudi moja kwa moja kwenye jambo lile lile, kama tu vile wana wa Israeli, walitaka mfalme ili mfalme huyu aweze kuwatawala na kuwafanya watende kama Waamori na Waamaleki na Wafilisti.

47 Mnajua, enyi mabibi, ya kwamba ni kosa kuvaa suruali? Mnajua jambo hilo? Mnajua ni kosa kukata vishungi vya nywele zenu? Je! Unajua ni kosa, ewe bwana, kwako kuendelea kuvuta sigara na kutenda jinsi unavyotenda? Je! Unajua ni kosa kwako kutokuwa mume wa nyuma yako, mke wako kushikwa na hamaki ndogo na kukufukuza nyumbani nawe unasema, "naam, nakutakia heri mpenzi, nitarudi moja kwa moja"? Unajua wewe … Unawezaje kuwa mlinzi wa Nyumba ya Mungu na huku hata huwezi kuitawala nyumba yako mwenyewe? Hiyo ni kweli kabisa. Je! Unajua, dada, ya kwamba mume wako si mume wako tu, bali yeye ni mtawala wako? Mungu alisema hivyo. Kwa sababu mume hakudanganywa, mwanamke alidanganywa. Nanyi wahubiri mtaendelea kuwafanya wanawake wachungaji na wahubiri makanisani mwenu, mkijua ya kwamba Neno la Mungu linahukumu jambo hilo.

48 Mtaendelea kutumia jina hilo "Baba, Mwana na Roho Mtakatifu" kubatiza, wakati hakuna hata chembe moja ya Andiko kwa ajili ya jambo hilo katika Biblia. Nataka askofu mkuu ama mtu mwingine anionyeshe mahali mtu ye yote katika Biblia aliwahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Ninataka mtu fulani anionyeshe mtu yeyote aliyewahi kubatizwa kwa njia yo yote mbali na Jina la Yesu. Lakini wa Yohana hawakuwa … wamebatizwa, walibatizwa wakiamini kwamba Yeye alikuwa anakuja, bali hawakujua Yeye alikuwa nani. Lakini mara walipotambua jambo hilo, iliwabidi kuja na kubatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo. Ninataka mtu fulani a … Ni—nimewauliza Assemblies of God, hao wahubiri wengine, Wabatisti, Wapresbiteri, na kila kitu. Hawataki, hawatazungumza juu ya jambo hilo. Nataka kuyaona hayo Maandiko.

Na kisha ati mimi ni "mshupavu wa dini," aha, halafu mimi ni "kicha," nimerukwa na akili, mimi ni "mwenda wazimu," kwa sababu tu kwamba ninajaribu kuwaambieni ile Kweli? Sasa, hilo—hilo ni uaminifu, enyi ndugu. Kama mtu amejitolea kabisa kwa ajili ya Mungu, umejitolea kabisa kabisa, kwa hali na mali. Wewe—wewe—wewe—wewe umewekwa wakfu, wewe ni—wewe ni kiumbe tofauti.

49 Wengi wameitwa, wachache wamechaguliwa. Naam, watu wengi wameitwa, unapata wito moyoni mwako, "Naam, naamini Mungu ananipenda. Naamini Yeye ananipenda."

Lakini, ndugu, hivi, utapotea kabisa kama hao wengine, kwa sababu watakuja huko siku hiyo, hata wakisema, "Bwana, nimetoa pepo katika Jina Lako. Nimefanya kila kitu kingine katika Jina Lako. Nimekuwa na ibada za uponyaji. Nimehubiri Injili. Nimetoa pepo."

Naye Yesu anasema, "Ondokeni hapa, hata siwajui, wanafiki. Ni Yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu!" Kwa nini watu hawawezi kuliona jambo hilo? Sasa, najua hilo linaudhi. Nami si—simaanishi kuwaumiza, sikusudii iwe hivyo. Lakini, ndugu, mimi—mimi …

50 Inaonekana kwangu kana kwamba tuko—tuko katika wakati wa mwisho, na Mungu anawafanya wana wenye mamlaka, akiwaeka katika mahali pao Kanisani, katika Mwili wa Kristo, Wake. Sasa, hakutakuwa na wengi sana ambao Yeye atawaweka mle ndani, nitawaambieni hilo kwanza. Unasema, "Loo, vema, kutakuwa na idadi kubwa sana!" Lakini Yeye amekuwa na miaka elfu sita ya kuwavuta watoke, pia. Kumbukeni, ufufuo unakuja nasi tunanyakuliwa pamoja nao. Wachache wao tu, mnaona. Wewe unatafuta wokovu wako, upesi. Jichunguze mwenyewe na uone ni kitu gani kimeharibika. Unaona? Angalia tu—kuna shida gani. Najua hilo—hilo ni gumu, lakini, ndugu, ni Kweli. Ni Kweli ya Mungu. Kufanywa wana wenye mamlaka!

51 Inatupasa kuw na juhudi sana kwa ajili ya Mungu, tunapaswa tukaze mwendo mchana na usiku. Hakuna kitu kinachopaswa kutuzuia, nasi tunapaswa kuwa watu waliokolea sana, na wema sana, na wema sana na wenye kufanana sana na Kristo maishani mwetu. Inatakiwa maisha ya kila siku. Yesu alisema, "Yatafakarini maua ya shambani, jinsi yakuavyo, kufanya kazi na kusokota; hata hivyo nawaambia ya kwamba Sulemani, katika fahari yake yote, hakuvikwa kama moja yao." Sulemani alikuwa na majoho yaliyopambwa kwa hariri ya fahari na mishono na kadhalika, lakini hilo—hilo halikuninii … hilo silo alilokuwa akilizungumzia. Ili ua likue, halina budi kufanya kazi mchana na usiku. Kwa nini unataka kurudi hapa kwenye mwisho wa mstari? Kama mwenye haki ataokoka kwa shida, na yule mwenye dhambi (huyo ni asiyeamini) na asiyemcha Mungu watakuwa wapi, mtu anayelisikia Neno na kukataa kutembea ndani Yake? Sasa tutafanya nini? Unaona? Sasa hiyo …

52 Hili ni, sasa, hili ni kanisa letu. Tuna labda wageni wanne ama watano miongoni mwetu. Lakini hili ni kanisa, ninawafundisha. Hili linarekodiwa kwenye kanda. Ninataka watu wanaosikiliza kanda, wakumbuke, hili ni kwa kanisa langu. Huko nje miongoni mwa watu huko ng'ambo, mimi hujaribu kuwa muungwana vya kutosha kuwaambia jambo hilo, kujaribu kukaa ambapo ningeweza kuwabembeleza kwa mawazo yao madogo sana ya maziwa mtindi. Lakini inapofikia hasa kuifundisha Kweli kikamilifu, hebu na tuifundishe.

53 Kufanywa wana wenye mamlaka, kuwekwa mahali pao! Wako wapi? Nionyeshe mahali walipo. Mungu akiwaita watoto Wake kando kwa njia ya udhihirisho. Haiwalazimu kusema neno moja juu yake, unaona jambo fulani limetukea. Akimweka mwanawe mahali pake, akimweka katika taratibu na mambo yale yale hasa. Yeye—yeye yuna mamlaka sawa, neno lake ni kama tu la Malaika Mkuu, bora zaidi. Mwana alifanywa mwana mwenye mamlaka, akawekwa mahali pa juu, akaketishwa pale, akabadilisha majoho yake, akabadilisha rangi zake. Baba yake alikuwa na sherehe, kasema, "Huyu ni mwanangu, tangu sasa

yeye ndiye liwali. Yeye ndiye mtawala. Yeye yuko juu ya urithi wangu wote. Yote niliyo nayo ni yake." Hiyo ni kweli. Ndipo tungeweza kurudi kwa yeye yule, Elah, Elah, Elohimu, Elohimu, unaona, ambapo Yeye anakaa peke Yake. Na kisha turudi kwa Yehova aliyeumba kitu fulani, Yeye alikapa mwanadamu mamlaka juu ya dunia. Tunangojea nini? Madhihirisho. Dunia inaugua. Hebu tulifikie tukalisome hilo. Vema.

> *… alitangulia kutuchagu … tufanywe wana kwa njia …* nafsi yake, *sawasawa na uradhi wa mapenzi yake,*
>
> *Na usif- … usifiwe utukufu wa neema yake, …*

54 Neema Yake ni nini? Kule nyuma hapo kabla, wakati Yeye hakuwa Baba; Neema Yake, upendo Wake, alijifanya Mwenyewe mtoto, kusudi tutangulie kuchaguliwa kufanywa wana wenye mamlaka, kwa utukufu wa neema Yake. Unaona?

> *… ambayo ametuneemesha* tukakubalika *ka—katika huyo* (Mtu) *mpendwa*, ambaye ni Kristo.

Alituneemesha vipi? Kwa nafsi Yake. Tunaingiaje ndani Yake? Kwa Roho mmoja, sote tumebatizwa katika Yeye. Sikilizeni.

> *Katika yeye huyo, kwa* (ile) *damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa d-h-a-m-b-i…*

55 Unawezaje kuhubiri kuchaguliwa tangu zamani, kwa Mungu kuamuru tangu zamani na kuwekwa, isipokuwa pawe na upatanisho wa dhambi mahali fulani? Mbona hivi? Kila siku unafanya makosa, kila siku unafanya mabaya. Lakini kama umezaliwa mara ya pili, mwanamume ama mwanamke, mara tu unapofanya kosa, Mungu anajua unalisikitikia. Ungeweza kusimama mbele ya—ya Rais Roosevelt au mtu mwingine yeyote, na kusema, "Nimekosea, Mungu nisamehe kwa jambo hili." Kwa nini? Na hapo ndipo ule upatanisho wa Damu …

Angalia hilo "d-h-a-m-b-i." Mwenye dhambi ni mwenye dhambi, hatendi dhambi. Lakini kanisa hutenda dhambi, linakosea, linapata wazo baya, dhana mbaya, hushikwa na wasiwasi, huyumbayumba kama mtoto mchanga anayetembea, akijaribu kujifunza jinsi ya kutembea. Yeye hajui jinsi ya kutembea vizuri bado, maana yeye ni mvulana mdogo. Lakini tuna Mkono unachuka chini kama sisi … unatushika na kutufanya thabiti, na kusema, "Piga hatua *hii* namna *hii*, mwanangu." Yeye hatuchukui na kutupiga kofi ati kwa sababu tulifanya kosa, Yeye hatupigi nusura tufe ati kwa sababu tunajifunza kutembea. Yeye anatupenda kama tunavyowapenda watoto wetu.

56 Baba halisi, halisi kabisa hangemchapa mtoto wake anapojaribu kutembea, kama akianguka sakafuni. Huinama na mkono mkubwa wenye nguvu na kumwinua, anamshike mikono miwili yake miwili, anasema, "Hivi ndivyo unavyofanya hilo, mwanangu. Tembea namna *hii*."

Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya Kanisa Lake! Huinama na kumshika kwa mkono Wake, anamwinua na kusema, "Tembea namna *hii*, mwanangu. Angalia huku, usi—usi—usiliseme namna hiyo, liseme namna *Hii*. Sasa, sijali kanisa linasema nini, Kile *huyu* anachosema, kile *yule* anachosema, wewe liseme kama *Hivi*. Namna *Hii*, hili ndilo Hilo! Kama Neno Langu linalihubiri, wewe dumu moja kwa moja Nalo, tembea nalo. Dumu moja kwa moja Nalo. Sijali yale kila mtu anayosema, dumu moja kwa moja Nalo. Tembea namna *Hii*. Hivi ndivyo unavyopiga hatua zako."

57 Dhambi zetu; upendo wa upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, la sivyo hatungepata nafasi. Jinsi ambavyo tungeweza kutia nanga kwenye Maneno hayo!

> *… sawasawa na wingi wa neema yake;*
>
> *Naye ali—alituzidishia …*

"Kuzidisha" ni nini? Loo, jamani! Naye *ametuzidishia*, "chungu nzima yake."

> *… alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi;*

"Ujuzi, hekima yote ametuzidishia sisi." Kwa "hekima" yote, si ya kilimwengu. Hekima ya ulimwengu ni upumbavu Kwake, na hekima ya Mungu ni upumbavu kwa ulimwengu. Ni kama tu mchana na usiku, mmoja hauwezi kukubaliana na mwingine. Lakini wakati jua linapoanza kuchomoza na mchana unakuja, usiku hutawanyika kutoka mahali mahali. Na wakati Nuru ya Injili inapoanza kuingia, mambo yote ya ulimwengu yanaanza kufifia. Na inafanya nini? Yeye huwazidishia Nuru ya Jua watoto Wake, wakitembea katika Roho, wakiongozwa na Roho wa Mungu, wakizidishiwa neema Yake, kwa ujuzi wote na hekima, ufahamu, na werevu kujua jinsi ya kutembea. Ukiona ni kosa, basi uwe mwangalifu kwa yale unayofanya, jinsi unavyo- … Kama ni kosa, uwe mwangalifu hata jinsi unavyoliendea. Ujuzi! Iweni karibu sana, na hakika kabisa ya kwamba mnajua jinsi ya kuliendea. Mwerevu kama nyoka, asiye na hatia kama hua. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.

58 Loo, hivi ni vito vya thamani, enyi marafiki! Tungeweza tu kukaa hapo siku baada ya siku. Hivi si ni vya ajabu? Ujuzi, hekima, Yeye ametuzidishia, akavimwaga! Si kutupatia kijiko kimoja, bali alichukua sepetu kubwa ya kuchotea na akaanza kutupakulia namna hiyo. Alituzidishia sisi, hekima pamoja na ujuzi wa neema Yake! Loo, neema ya ajabu, jinsi ilivyo tamu ikisikika!

> Sasa, *naye* ametuzidishia *hiyo hekima yote … ujuzi;*
>
> *Akisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, …*

Yeye anazungumza na nani? Madhehebu? Tafadhali, ndugu zangu, msifikiri ninayadharau madhehebu yenu, sivyo. Ninajaribu kuwaambia kilikuwa ni kitu kibaya tangu mwanzo. Yesu alisema, "Enendeni mkaihubiri Injili," tukaondoka tukaenda na kuunda madhehebu. Hiyo ndiyo sababu hatuna kitu Hicho, tunatembea kwa hekima ya mwanadamu. Laiti Calvin angeweza kufufuka!

59 Mbona, nilisimama si muda mrefu uliopita karibu na kaburi la mtu mashuhuri, mtengenezaji mkuu. Nami nikawaza, jinsi alivyokuwa mtu mkuu! Alikuwa hivyo! Vema, ili … Sitaninii … Ilikuwa ni John Wesley. Nami nikawaza, kama John Wesley angeweza kufufuka kutoka kwenye kaburi hili leo na kuona hali ya kanisa lake, angelionea haya jina lake. John Wesley alikuwa mcha Mungu, kinga iliyonyakuliwa, kama alivyokiita. John Wesley alikuwa mtu mtakatifu aliyemwamini Mungu, na akamfuata hatua kwa hatua. Lakini baada ya John kufa, wao walisema, "Tutaunda kanisa la John ili tuwe na kanisa, nasi tutaliita kanisa la Kimethodisti kwa sababu ya mtindo wake wa utakaso kwamba ndii kazi ya pili ya neema."

Ndipo wao wakaunda kanisa, na leo hao wafuasi wa kanisa wanakana kila kitu ambacho John Wesley alikisimamia. John Wesley alihubiri uponyaji wa Kiungu. John Wesley aliamini katika ubatizo wa Roho. John Wesley aliamini katika kurejeshwa kote kwa vipawa. John Wesley, Martin Luther, wengi wa hao watu mashuhuri walinena kwa lugha na kufasiri. Na, leo, ungenena kwa lugha katika kanisa la Kimethodisti ama kanisa la Kilutheri, wangekufukuzia nje. Kuna nini? Wakati ule ule tunaopaswa kuwa tukiweka wana mahali pao, kuna nini? Wao wameingiza kitu kingine, kwa sababu hawajui siri ya Mungu. Nao kamwe hawataijua kupitia kwenye seminari!

60 Hebu niwasomee tu jambo fulani. Ni sawa? Vema. Hebu na tufungue, nimeandika kitu fulani hapa. Hebu na tuone jinsi Paulo … Sasa, hapa, huyu hapa mwalimu wa Ujumbe huu. Hebu na tuende kwenye Matendo 9:5, kwa muda kidogo tu. Sikilizeni jinsi Paulo alivyopata Ufunuo huu, chochote kilichotukia. Sasa, katika Matendo 9 tunaanza kusoma, namna hii. Hili ni darasa la shule ya Jumapili, hivyo kwa nini basi—mbona tusilisome? Hebu nijue nitakapomaliza …?…

> *Na Sauli, akizidi kutisha na kuwaza* … (Loo, maskini Myahudi huyo mwenye hasira, na mwenye hamaki, na pua kama ndoana!) … akiwaua *wanafunzi wa Bwana, akamwendea kuhani mkuu, akataka ampe barua za kwenda Dameski zizlizoandikwa kwa* sinagogi, *ili akiona watu …*

"Nitaenda nikawatafute! Kama nikiweza tu kuwapata, jamani, kile nitakachowatendea! Mnaona, kama nitaweza tu kuwapata!" Bali alikuwa amechaguliwa tangu zamani!

61 Unajuaje kama huyo maskini muuza chang'aa hapa chini hakuchaguliwa tangu zamani kwa ajili ya Uzima? Unajuaje kama yule maskini kahaba ambaye hata hutaongea naye, unajuaje kwamba kupeana mkono naye kidogo na kumwalika kanisani hakutamfanya yeye mtakatifu wa Mungu, kule Utukufuni? Wakati … Unajuaje sivyo alivyo? Hilo ndilo tusilolijua. Lakini huo ni wajibu wetu. Kama vile mvuvi alivyotupa jarife baharini na kuvuta, yeye alivua vyura, samaki, mijusi, buibui wa maji, na kila kitu kingine, lakinibaadhi yao walikuwa samaki. Hakujua, yeye alitupa tu jarife. Hivyo ndivyo tunalofanya. Mwangalie Paulo.

> … akitaka *barua za kwenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi, ili akiona watu wa njia hii, waume au wake,* awalete wamefungwa *Yerusalemu*. (Ndugu, yeye alikuwa mjeuri kweli!)
>
> *Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski, ghafla ikamwangazia …*

62 Pakatokea kasisi anakuja barabarani, Daktari F. F. Jones, na kumwambia, "Unahitaji u-ujuzi wa seminari sasa, mwanangu, na ninaamini Mungu angeweza kukutumia"? Hilo si lingekuwa ni Andiko la kuchukiza sana, kulisoma namna hiyo? Sasa, hilo lina maana tu kama … Sisemi hivyo kwa utani. Hilo ni, sisi, hilo lina maana tu sawasawa na vile tunavyolielewa jambo hilo leo. "Unajua, mama yako alikuwa mwanamke mzuri, naamini wewe ungekuwa mhubiri mzuri." Tazama yaliyotukia.

> *Hata-hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafla ikamwangaza* kila mahali nuru … (whiu, inaanza kwa ya kimbinguni) … *nuru kutoka mbinguni*:
>
> *Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia … Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?*
>
> *Akasema, U nani wewe, Bwana? Naye* Bwana akamwambia, *Mimi ndimi Yesu unayenitesa wewe;* na *ni vigumu kwako kuipiga teke* michokoo.

> Akatetemeka, na kushikwa na hofu, kisha akasema, Bwana, wataka nifanye ... nini? Naye Bwana akamwambia, *Simama, uingie mjini, nawe utaambiwa* yakupasayo kutenda.

63 Na hao watu wakasafiri pamoja naye, wakasonga mbele, kisha wakamkuta mtu fulani. Anania, kule chini, aliona ono. Yote ya kimbinguni! Naye maskini Sauli, huyo maskini jamaa mkorofi! Huyu Anania aliona ono, akaangalia nyumbani mwake. Alikuwa nabii, katika nyumba yake akiomba, naye akaona ono. Yeye … Bwana akanena naye na kusema, "Kuna mtu anayeshuka akija barabarani kule, kipofu tu kama popo, na jina lake ni Sauli, yeye ni Sauli wa Tarso."

Akasema, "Bwana, nimesikia mambo makuu. Usinitume, mimi ni mtu mdogo. Usinitume nikamtafute."

Akasema, "Lakini, tazama, alipokuwa njiani akija, nilimwonyesha ono. Nilimtokea katika Nguzo ya Moto. Nilimpiga kwa upofu sana awezavyo kuwa. Nami ilinibidi kumpofusha na kumrarua kabla sijaweza kumtumia. Unaona, ilinibidi kurarua theolojia yake yote. Uajua, yeye alikuwa—alikuwa—alikuwa ni jamaa mashuhuri katika moja ya makanisa hayo kule. Yeye alikuwa na kila aina ya shahada, haikumlazimu kulainisha chochote, lakini,"Yeye akasema,"kilichonipasa kufanya ni kuondoa yote ndani yake."

64 Hilo ndilo lililokuwa jambo lenyewe. Haikuwa kumwongezea mengine ndani yake, bali kuyatoa ndani yake. Nafikiri hiyo ndiyo shida ya makasisi wetu wengi leo hii; ondoeni ndani yenu, ambapo Mungu anaweza kuwatia Roho Mtakatifu ndani yao. Toeni! Hapo, yeye alisema yeye …

Naye akasema, "Bwana, lakini huyu—huyu—huyu mtu ni mtu mbaya sana."

Yeye akasema, "Lakini, tazama, yeye anaomba. Sasa, utashuka kupitia barabara fulani na kisha ufike kwenye kisima fulani. Upite kisima hicho upande wa kushoto, kisha uteremke. Kutakuweko na nyumba nyeupe, nenda ukabishe hodi mlangoni. Yeye amelala tu mle ukumbini, huko ndiko walikoweza kumfikisha. Mwekee mikono yako, mchukue umpeleke kwenye mto wa Dameski na umbatize katika Jina la Yesu. Maana, nakwambia yale nitakayofanya, yeye atateswa kwa mambo mengi kwa ajili Yangu, kwa kuwa yeye ni mjumbe Wangu kwa Mataifa." Amina!

65 "Vema, sasa, ngoja kidogo, Bwana! Sasa, nimshauri akasome shule gani?" Nitawaambieni tutakalofanya, hebu tusome Wagalatia tuone. Sura inayofuata tu—sura iliyotangulia papo hapo nyuma. Hebu tufungue Wagalatia 1, na tuanzie kwenye aya ya 10, na hebu tuone ni shule gani Paulo aliyoenda, ni seminari gani, na ni mikono ya nani aliwekewa, na, loo, yote hayo yaliyotukia. Wagalatia sura ya 1. Kuokoa wakati, hebu tuanze kuhusu kuongoka kwake, aya ya 10.

> *Maana sasa je! ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nikiwapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.

Loo, jamani, jamani, jamani! Hebu niseme jambo fulani dogo kabla ya hili hapa. Wagalatia 1, chukua sura ya 8. Ni wangapi wanaojua kwamba Paulo ndiye aliyewafanya hao watu wabatizwe tena katika Jina la Yesu, Matendo 19? Hakika alifanya hivyo. Hebu tuchukue tu hapa juu kidogo tu hapa, aya ya 8—ya 8.

> *… ijapokuwa sisi, au malaika wa mbinguni, atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe.*

Uliipata wapi Injili hii, Paulo? Ile aya ya 9.

> *… tulivyotangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yoyote, isipokuwa hiyo mliyosikia, tuliyowahibiri, na alaaniwe.*

Kama yeye ni malaika mkuu, kama yeye ni askofu, kama yeye ni mwangalizi mkuu, kama yeye ni Daktari *Fulani*, hata awe nani, iwapo hahubiri ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, ubatizo wa Roho Mtakatifu, hahubiri kurejeshwa kwa karama, Kuja kwa Kristo, mambo haya yote, na alaaniwe! Kama akijaribu kuchukua moja ya hili Neno hapa na kusema lilikuwa kwa ajili ya siku nyingine na kuliweka kule kwenye wazo motomoto tulilofunzwa kwenye seminari fulani, na alaaniwe!

66 Hebu na tuendelee kusoma, tuone jinsi Paulo alivyolipata, mwone jinsi, ninayojaribu kuwaambia asubuhi ya leo.

> *Maana sasa je! ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu,* basi mimi *singekuwa mtumwa wa Kristo.*

Nawezaje kutarajia chochote, anawezaje mtu anayempenda Mungu, na mhubiri, hasa, kutarajia kufanya jambo lolote ila kuchukiwa na mwanadamu? Watu watakuchukia. Vema, wao walisema … Yesu alisema, "Kama wakiniita Mimi, Bwana wa nyumba … Mimi ndiye Bwana, aliye mkuu kuliko ninyi nyote. Mimi Ndimi ninayeweza kufanya miujiza mingi zaidi na kufanya mengi zaidi kwa Roho Mtakatifu kuliko ninyi nyote, kwa sababu nina utimilifu wote ndani Yangu. Na kama wameniita Mimi 'Beelzebuli,' na ninyi

watawaita mara ngapi zaidi? Lakini," kasema,"msifikiri-fikiri mtakayokuwa mkisema, kwa kuwa si ninyi mtakaokuwa mkinena, itakuwa ni Baba anayekaa ndani yenu, atakayekuwa akinena wakati huo. Dumuni tu na Neno." Na Yeye, alipomaliza kukiandika kile Kitabu, alisema, "Mtu ye yote atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Kitabu hiki au aongeze neno moja Kwake, huyo ataondolewa katika Kitabu cha Uzima, kwa ajili yake." Mungu na atusaidie kudumu Nalo moja kwa moja!

67 Sasa ile aya inayofuata, hebu nisome sasa, nisome upesi sasa.

> *Lakini nawajulisha …* Hiyo ni kusema, kuwatia hukumuni. *Ndugu zangu, Injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu.*

Sasa, mimi si Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, wala Mpentekoste; wala haikutoka kwa mwanadamu. Wala …

> *Kwa uwa sikuipokea kwa mwanadamu, wala sikufundishwa, …*

"Sikuipokea kamwe kutoka kwa mwanadamu, si seminari, hakuna daktari, si uungu, si shule ya elimu. Kamwe sikuipokea hivyo, kamwe sikuifundisha hivyo, kamwe sikuipata hivyo, haikunijia hivyo." Ilikujaje basi, ewe Paulo?

> *… bali kwa ufunuo wa wa Yesu Kristo.*

"Wakati Kristo alipojifunua Mwenyewe kwangu, ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu, wakati ile Nguzo ya Moto iliposhuka juu yangu siku hiyo, nilisema, 'U nani Wewe, Bwana?' Yeye akasema, 'Mimi ndimi Yesu.'"

68 Sasa, nitawaonyesha kile—kile kilichompata. Sasa, sasa hivi kama jamaa yeyote amepata ujuzi, wangetaka kumpa miaka kumi akajifunze Kiyunani, na miaka kumi zaidi kujifunza kitu kingine, na kufikia wakati huo amekwisha. Tazama.

> *… sikuipokea kwa mwanadamu, wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.*

> *Maana mmesikia habari za* mazungumzo *yangu zamani katika dini ya* Kiyahudi, …

"Nilikuwa daktari mkubwa, nakwambia. Nilipata kitu halisi." Alifundishwa chini ya Gamalieli, mwalimu bora kuliko wote waliokuwa nao nchini. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Gamalieli alikuwa mmoja wa waalimu bora, bora kuliko wote? Naam, bwana. "Dini yangu ya Kiyahudi, nakwambia, ilikuwa imetia fora; nilijua kabisa jinsi ya kukariri Imani ya Mitume na mambo hayo yote, mnaona. Nilijua jinsi ya kukariri maombi yote ya asubuhi na kuwabariki watu." Unaona?

> *… kwamba* wakati huo *nililitesa kanisa la Mungu kupita kiasi, nikaliharibu*: Jinsi ambavyo nilijaribu kulikomesha kundi hilo la watakatifu wanaojivingirisha! Unaona? Unaona?

> *Nami naliendelea katika dini ya* Kiyahudi …

"Nilikuwa mtu mashuhuri. Nakwambia, kweli mimi … Niliendelea, niliwaonyesha ningeweza kuwapondaponda, kwa kuwa nilimwua Stephens na mambo mengine kadha niliyotenda. Angaliani jinsi nilivyotenda!" Jinsi ambavyo alitesa kupita kiasi!

> *Nami naliendelea katika dini ya* Kiyahudi *kuliko wengi walio hirimu yangu katika taifa langu, nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zao.*

69 Sasa, kumbukeni, si Neno la Mungu, "mapokeo ya baba zao," mapokeo ya kanisa, kwa maneno mengine. "Nadhani nilikuwa Mmethodisti kabisa, nilikuwa Mbaptisti wa hali ya juu, nilikuwa Mpentekoste kabisa." Loo! Mimi nataka niwe Mungu kwa hali na mali. Naam, hivyo ndivyo ilivyo. Unaona? Vema.

> *… mapokeo ya baba zangu.*

> *Lakini ilipompendeza Mungu,* … (loo, loo, Paulo, unasema hivi) … *aliyenitenga tangu tumboni mwa mama yangu,* ambaye hata alinileta humu ulimwenguni, *akaniita kwa neema yake,*

> *Kumfunua Mwanawe ndani yangu, …*

Vipi hilo? "Roho Mtakatifu ndani yangu! Ilimpendeza Mungu kunichukua, aliyenitenga tangu kwenye tumbo la uzazi, na akanipa Mwana, ambaye ni Roho Mtakatifu katika umbo la Roho, ndani yangu, kujifunua Mwenyewe kwangu." Loo, jamani! Whiu! Na—na—naamini nataka kupaza sauti kidogo tu.

70 Angalia, hebu nikwambie, ndugu. Wakati ilipompendeza Mungu! Loo, haleluya! Wakati ilipompendeza Mungu! Baba mlevi. Mama … Mungu akubariki, mama, sisemi neno dhidi yako. Lakini mama asiyejua Mungu zaidi ya sungura anavyojua juu ya viatu vya theluji. Na baba ambaye alilala mitaani amelewa. Na bila

hata viatu vya kuendea shuleni, na nywele ndefu zilizoning'iniashingoni mwangu, na kila mtu alinichukia kwa sababu nilikuwa Mkentucky hapa Indiana. Na jinsi, loo, jinsi nilivyokuwa naonekana ni kitu kinachonuka. Lakini ilimpendeza Mungu! Amina! Ilimpendeza Mungu, ambaye alinitenga tangu tumboni mwa mama yangu, apate kumfunua Mwanawe ndani yangu, kwa kunifanya mhudumu wa Neno, ambaye angedumu moja kwa moja na Hilo, ambaye angeonyesha maono na ishara na maajabu na miujiza. Na, loo, jamani!

71 Mnaona kile alichokuwa akizungumzia? Ilimpendeza Mungu kufanya hivyo! Vipi? Sikilizeni kwa makini. "Kumfu- …" Chukueni aya ya 16 sasa.

> *Kumfunua Mwanawe ndani yangu, ili niwahubiri Mataifa habari zake; mara sikufanya shauri na* kanisa.

"Kamwe sikwenda kwa askofu yeyote na kumwuliza nipaswalo kufanya. Kamwe sikuwaendea watu wenye mwili na damu, madhehebu yo yote ama cho chote kile. Sikuwahi kuwa na uhusiano wowote nao. Kamwe sikufanya shauri na watu wenye mwili na damu. Wala sikupanda kwenda Yerusalemu kwa hao makuhani wote watakatifu na baba watakatifu, na hao wote, na kusema, 'Sasa, mnajua, nilipata ono, nifanye nini juu yake? Nilimwona Bwana Yesu mbarikiwa katika ono.' Wao wangesema, 'Ondoka hapa, wewe! Nini … Ewe watakatifu anayejiviringisha! Vema, umepatwa na nini?' La, kwanza nilikuwa na digrii zao zote. Nilikuwa …"

72 Na Paulo akasema hapa, naweza kuwaonyesha katika Maandiko, kwamba alisema ilimbidi kusahau yote aliyowahi kujifunza, na kuyahesabu kama si kitu, kusudi apate kumjua Kristo. Loo!

> *Wala sikupanda kwenda Yerusalemu kwa hao waliokuwa mitume kabla yangu; bali nalikwenda Arabuni, kisha* nikageuka *nikarudi tena Dameski.*
>
> *Kisha baada ya miaka mitatu, nalipanda kwenda Yerusalemu ili nionane na Petro, nikakaa kwake siku kumi na tano.*

Na tunapoendelea kusoma, tunaona ya kwamba yeye na mtume Petro hawakuwa wameonana maishani, hawakujuana, hawakuwa wameonana, lakini walipokutana walikuwa wakihubiri Injili ile ile. Mungu ana shule. Unaona? Naam!

73 Huyu hapa Petro, alisimama kwenye Siku ya Pentekoste, kasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

Filipo alisema, "Loo, jinsi hili lilivyo na utukufu! Sina budi kufanya jambo fulani pia. Huko chini … Nina wito wa kushuka kwenda Samaria." Akashuka akaenda kule na kuanza kushuhudia mtaani. Muda si muda, akatokea mgonjwa, akamwekea mikono, naye akaanza kuruka na kurukaruka. Kasema, "Utukufu kwa Mungu, tumewasili!" Akaanza kuwa na mkutano mkubwa. Akasema, "Nyote mnahitaji Roho Mtakatifu." Akasema, "Liwapasalo kufanya, hamna budi kubatizwa katika Jina la Yesu." Kwa hiyo akawachukua, kila mmoja, huko nje na kuwabatiza wote katika Jina la Yesu. Kasema, "Njoo, Petro, weka mikono yako juu yao sasa." Nao wakampata Roho Mtakatifu.

Petro, huko juu kwenye nyumba ya Kornelio, vivyo hivyo.

74 Paulo hakuwa amewahi kumwona wala kusikia neno juu yake. Bali alipitia pande za juu za pwani ya Efeso, naye akawaona wanafunzi fulani. Akakutana na mhubiri Mbaptisti, ndivyo alivyokuwa, Apolo, mwanasheria aliyeongoka, mwerevu, mwenye akili nyingi, akichukua Agano la Kale na kuthibitisha kwa Hilo ya kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Naam, bwana, yeye alikuwa mtu mwerevu. Nao walikuwa wakipaza sauti, walikuwa na shangwe. Biblia ilisema hivyo. Soma sura ya 18 na 19 ya Matendo uone kama hilo si kweli. Walikuwa na furaha, walikuwa wakicheza katika Roho, na wakikimbia huko na huko, mwajua. Paulo alisema, "Lakini je! Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

75 Na kwenu ninyi ndugu wa Kibaptisti mnaojaribu kusukumiza jambo hilo kwenye koo la watu, na kusema Kiyunani asili kilisema, "Je! Mlipokea Roho Mtakatifu tangu tangu, au *wakati* mlipoamini?" Nawapa changamoto mniletee hicho Kiyunani! Mimi mwenyewe ninacho Kiyunani cha asili. Nina Kiaramia pia, na Kiebrania, pia. Kila moja inasema, "Je! Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Kwa imani unaokolewa, hiyo ni imani yako kwa Mungu. Ile Damu inawasafisha mbali na dhambi, kwa sababu inatoa sadaka. Damu haikuokoi, Damu inakuweka kuwa msafi. Unasemaje kwamba umeokolewa? Kwa imani umeokolewa, na hilo ni kwa kujua kwa Mungu tangu zamani, akikuita. Umeokolewa, na Damu inafanya upatanisho, ikikuweka msafi daima. Na kisha kwa Roho mmoja unabatizwa katika Roho Mtakatifu, ukaingizwa katika ushirika wa waamini, na katika ushirika wa Roho Mtakatifu, kuongozwa na Roho, ukifanya ishara, maajabu.

76 Ngojeni, tutayafikia, tukingojea kitu fulani, muda kidogo tu nasi tutakipata, natumai tutakipata hata

hivyo. Niliwaambia mniite wakati huu, sivyo? Imetokea tu kwamba niliiangalia. Neno—neno moja tu ama mawili zaidi. Ninii tu … Ni—ni kidogo tu zaidi.

77 Wokovu huu unadumu muda gani, muda gani? Ni wokovu wa aina gani? Kutoka kanisa moja hadi kanisa lingine? Kutoka … Hebu tufungue Waebrania 9:11, kwa muda kidogo tu, tu—tuone tu ni muda gani, kwa dakika chache tu. Fungueni Kitabu cha Waebrania na hebu—hebu tuone wokovu huu utadumu muda gani. Tuone ni aina gani ya wokovu. Hebu tusome sasa Waebrania 9:11.

> *Lakini Kristo, akiwa kuhani aliye mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake*, … (sasa huyu ni mwalimu yule yule, Paulo, mnaona) … si ya jengo … *jengo hili;*
>
> *Wala si kwa damu ya mbuzi* wala *ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja* (mara ngapi? Moja!) kwneye *Patakatifu, akiisha kupata …* (wokovu wa wiki moja, wokovu wa kudumu mpaka uamsho unaofuata? Ni wa namna gani? ) … *ukombozi wa milele kwa ajili yetu.*

78 Neno "Milele" lina maana gani? Katika Kristo, baada ya mimi kuamini … Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu, "Kristo," ila kwa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo kuna tabaka tatu za watu: wasioamini, wanaojifanya waaminio, na waaminio. Lakini hao walioamini hata kupokea Uzima wa Milele, wameingia nyuani.

Chukueni lile hekalu la kale, jambo la kwanza walilofanya lilikuwa nini? Waliingia kwenye nyua, Mataifa. Iliyofuata ilikuwa ile madhabahu ya shaba, mahali walipoiosha dhabihu kwenye birika la dhahabu. Lililofuata lilikuwa kuchinjwa kwa ile dhabihu, na kunyunyizia damu juu ya madhabahu. Halafu, mara moja kwa mwaka, Haruni akiishatiwa mafuta, loo, (kwa nini?) kwa manukato ya Waridi la Uwandani, kwa mafuta ya thamani yaliyokuwa na manukato, waliyamwaga kichwani mwake, yakatiririka hata kwenye pindo za mavazi yake. Angalia jinsi mtu huyu alivyopaswa kuingia mle ndani nyuma ya hayo mapazia, mara moja kwa mwaka, akibeba mbele yake damu kwa ajili ya Kiti cha Rehema. Naye katika mwaka mmoja akaingia na fimbo yake mle na kuisahau. Waliporudi kuichukua, tayari ilikuwa imechipuka na kuchanua. Fimbo ya kale ambayo labda alikuwa ameibeba miaka arobaini kule jangwani, iliyokuwa imewekwa Mahali pale Patakatifu! Tazama, wakati wao walipochukua ile damu ya agano, ile damu, yeye alitiwa mafuta. Naye alikuwa na mavazi yaliyokuwa na njuga ndogo za kuliza ndani yake, komamanga na njuga. Na mtu huyo ilibidi atembee hivi kwamba kila aliposogeza mguu wake, na kusogea *hivi* na kupiga hatua, ziliimba "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana." Loo, jamani!

79 Ninazungumzia nini? Lisikieni, enyi Maskani ya Branham! Mmekuwa na nafasi yenu. Mara mtu anapotiwa mafuta na Roho Mtakatifu, apate kufanywa mwana mwenye mamlaka katika familia ya Mungu, apate kuwekwa mahali pake na Baba, na kutumwaa katika huduma hapa nje, katika kusudi lake la maisha, ama kile Mungu alichomwitia, mwenendo wake sharti uwe "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu!"

"Loo, huna budi kugeukia upande *huu* na uwe …"

"Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana."

"Loo, huna budi kuamini yote aliyo mzee, *haya*."

Lakini, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana." Acha Neno Lake liwe la kwanza, hebu liwe kila kitu kilichopo, likolee, liwe limekaa moyoni mwako! Mwenendo wako unapaswa kuwa katika Neno. "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana."

"Loo, laiti unaglikuja tu hapa! Nitakwambia tutakalofanya, tutaunda dhehebu, tukuweke katika dhehebu letu, utakuwa mtu mashuhuri."

"Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana," ukisonga mbele. Haileti tofauti yo yote yale mtu yeyote asemayo!

"Agiza hizi kanda hizi zirudishwe! Fanya *hivi*, fanya *hivi*, fanya *vile*, fanya *vile*, *vinginevyo*."

"Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana." Umeelekeza macho yako kuelekea Kalvari, na hakuna kitu kitakachokuzuia! Mwenendo halisi wa maisha yako, unatembea kwenye Barabara Kuu ya Mfalme, umetiwa mafuta na Mafuta kwa Mafuta ya thamani, ukielekea kwenye Patakatifu pa patakatifu. Whiu! Amina. Vema.

80 Paulo alisema hakulipata Hili kutoka kwa mwanadamu. Sasa yeye anasemaje, tukirudi kwenye Wagalatia, somo letu. "Akiisha kutujulisha siri ya mapenzi Yake." Mapenzi Yake ni nini? "Akatujulisha siri za mapenzi Yake." Ninyi mnaoandika, aya ya 9. Sasa nitaharakisha upesi sana nimalize hili, maana tunachelewa.

Loo, kila Neno ni kama kwamba …?… Loo, kila Neno ni kito cha thamani. Unaweza tu kulichukua na kuendelea kulifafanua kindani. Unaweza kuchimbua, naweza … Unaweza kuchukua Neno moja la hayo Maneno mle, ulipeleke hadi Mwanzo na ulifafanue kindani, ulipeleke kwenye Kutoka na ulifafanue tena, unaweza kulipeleka kwenye Mambo ya Walawi na kulifafanua tena, na, wakati unapofikia kwenye Ufunuo, Hilo ni Yesu kwa kila kipengele! Amina. Unaweza tu kulifafanua kindani kiasi utakavyo, litakuwa Yesu utakapofikia—unapofikia Ufunuo. Kwa kuwa, Yeye alisema, "Mimi Ndimi Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja. Mimi ndimi niliye Shina na Mzao wa Daudi, ile Nyota ya Asubuhi. Mimi ndimi Alfa, Omega." Hiyo ni kusema, A na Z katika alfabeti za Kiyunani. "Mimi ni kutoka A hadi Z. MIMI NIKO! Mimi ni Yote-katika-yote." Hiyo ni kweli. "Mimi ndimi niliyekuwa hai na niliyekuwa nimekufa, na ni hai milele. Ninazo funguo za mauti na kuzimu." Loo, jamani! Kila kito cha thamani unachochukua hapa na kuanza kukisugua, kitasugulika kuwa Yesu.

81 Sasa, baadaye kidogo tu na ndipo tuta—tuta—tuta—tuta—tutakoma. Naam. Tunangojea nini, basi? Kwa nini mko hapa mkutanoni? Kusudi lake ni nini? Ulimwengu unaugulia kwa sababu gani? Bomu la atomiki linaning'inia kule kwa ajili gani, zile molekuli na atomi ni nini? Na, loo, yote yanahusu nini?

Fungueni, Warumi 8, kwa muda kidogo tu. Inangojea nini? Haya yote yanangojea nini? Ni saa ngapi? Warumi, sura ya 8, na hebu tuanze na kusoma kwenye, loo, ningesema ya nane- … Hebu tuanzie kwenye ile ya tisa- … aya ya 19, na ninii tu—tusome tu papa hapa kwa ajili ya kupafanya, panapoifanya tamu hasa. Hiyo ni kweli. najua mnakoelekea hapo. Vema. Warumi, sura ya 8, naamini niko sahihi sasa. Naam, bwana. Sura ya 8, na hebu tuanzie hapa kwenye aya ya 18. Hebu tuanzie tu kwenye aya ya 14.

> *Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio … wana wa Mungu.* Hiyo ni kweli.
>
> *Kwa kuwa hamkupokea tena Roho ya utumwa iletayo hofu; …*

82 "Loo, sijui kama naweza tu kushikilia. Oooo, laiti ningalishikilia sasa!" Usishikilie kitu chochote! Si ati kama mimi nilishikilia, ni kama Yeye alishikilia. Mimi niko ndani Yake sasa, unaona.

Vema, unasema, "Vema, kama niko ndani Yake!" Sasa ninyi—ninyi Wapresbiteri mnasema, "Aha, daima tuliamini jambo Hilo." Lakini maisha yenu yanathibitisha kwamba hamumo, isipokuwa mtembee katika maisha yale Yeye aliyotembea, mnaamini Injili ile ile aliyohubiri.

Mnasema, "Aha," Mbaptisti aseme, "hakika, naamini katika usalama wa Milele." Na utoke nje hapa na kuvuta msokoto wa sigara na kukimbia kwenda kwenye dansi, na wanawake wakate nywele zao, wapodoe nyuso zao na kutenda sijui kama kitu gani? Matunda yako yanathibitisha kwamba huliamini Hilo.

Ninaposema, "Je! Unaamini katika uponyaji wa Kiungu?"

"Loo, Daktari Jones alisema ilikuwa hivyo, kwa hilo lilikuwa katika siku za nyuma."

Sasa, ewe mnafiki! Una shida gani? Wewe maskini mtoto uliyedanganyika vibaya. Uko mbali sana na Injili hata inasikitisha. Umepoongozwa vibaya ukaelekezwa kwenye barabara fulani ya matope kuelekea kwenye jalala linaloungua. Hivi huoni Yeye alivyosema hapa? Kwamba, kila roho inayokiri kwamba Yesu hajaja katika mwili sasa hivi, ni roho mbaya. Biblia ilisema Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kile Yeye alichosema wakati huo, ndivyo alivyo sasa, daima atakuwa hivyo. Sikilizeni tu.

> *Kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali mlipokea Roho* ya- …

[Kusanyiko linasema, "*kufanywa wana wenye mamlaka.*" — Mh.]

83 Sasa, ukiisha kufanywa mwana mwenye mamlaka, vema, ukiisha kufanywa mwana mwenye mamlaka. Unawekwa mahali pako, ndipo unafahamu, baada ya kufanyika kwa sherehe na umewekwa katika ule Mwili ipasavyo. Wewe ni mwana, hakika, binti, unapozaliwa mara ya pili ndivyo ulivyo, huko ndiko kuzaliwa kwako. Lakini sasa unawekwa mahali pako.

> Hatujapokea *roho iletayo hofu; bali tulipokea Roho, tumepokea Roho wa kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, Baba*. Ambayo maana yake ni, "Mungu wangu." Vema.
>
> *Roho mwenyewe* anashuhudia *pamoja na roho zetu, ya kuwa* tu—tu *watoto wa Mungu*:

Hilo linafanyaje? Unasema, "Utukufu kwa Mungu! Haleluya! Hainisumbui, mimi ni mwana wa Mungu," na unaondoka unakwenda kufanya mambo unayofanya? Roho wa Mungu atafanya kazi za Mungu.

Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Unaona? Unaona?

84 Kama—kama—kama—kama mzabibu huu ukichipuka na kuzaa vishada, na unaofuata unachipuka na kuzaa vishada vya maboga, kuna kasoro fulani. Unaona? Ni kanisa lililopandikizwa, ni mzabibu uliopandikizwa, ni mtu aliyepandikizwa. Kama mtu ni wa dhehebu fulani, ni mfuasi wa dhehebu fulani na wanajiita Mkristo, na hana Roho Mtakatifu na hana Nguvu za Mungu na mambo haya yote …

85 Sasa, kama ukiondoka uende nje hapa na kutenda kama kundi la hawa waliolewa, ati kwa sababu tu ulinena kwa lugha. Nimewaona mapepo yakinena kwa lugha. Naam, bwana. Nimeyaona yakicheza katika roho, na kupiga makelele na kutoa povu kinywani, na kila kitu kingine, na yote hayo. Nimeona hayo. Mimi ni … Mimi sizungumzii jambo hilo. Ninazungumza juu ya Roho wa Mungu.

*Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwasisi … watoto wa Mungu;*

*Na kama basi ni watoto, tu warithi; warithi wa Mungu, … warithio pamoja na Kristo; naam … tukiteswa pamoja naye, ili … tupate kutukuzwa pamoja naye.*

*Kwa maana nahesabu mateso …*

Sikilizeni tu jambo hili. Loo, kama hili si zuri!

*Kwa maana nahesabu mateso ya wakati huu wa sasa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu.* Ndani yetu!

*Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi…*

Inalita hapa, ina—ina neno dogo pale, neno dogo hapa pembezoni, "uumbaji" ni sahihi, katika Kiyunani.

… hutazamia kwa uumbaji, uumbaji unangojea madhihirisho *ya wana wa Mungu.*

86 Kila kitu kinangojea nini? Uumbaji wote unangojea nini? Madhihirisho ya wana wa Mungu. Unangojea Kanisa liingie mahali pake. Ni nani aliyekuwa mwana wa Mungu, wakati Adamu, milki yake ilikuwa wapi? Dunia. Yeye, yeye alikuwa na mamlaka juu ya nchi. He, hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." —Mh.] Yeye hakuwa Elah, Elah, Elohimu wakati huo; Yeye alikuwa Yehova. Unaona? Hiyo ni kusema, "Mimi ndimi Mungu, na nimewafanya miungu wadogo chini yangu. Nami nimewapa mamlaka. Na katika milki yao, utawala chini yao, ni dunia." Mwanadamu alikuwa na mamlaka juu ya nchi. Na uumbaji wote unangojea watoto wa Mungu wadhihirishwe. Loo!

Tunakutazamia kuja kwa siku ile ya furaha ya ule Utawala wa Miaka Elfu,
Wakati Bwana wetu aliyebarikiwa atakapokuja na kumnyakua Bibi-arusi Wake anayengojea;
Loo, dunia inaugua, inalia kwa ajili ya siku ile ya kufunguliwa kutamu,
Wakati Mwokozi wetu atakaporudi duniani tena.

87 Je, hiyo ni kweli? Kutazamia. Mungu akijaribu kuliweka kanisa Lake mahali pake, kujidhihirisha Mwenyewe, akimpata mmoja anayeweza kutenda kazi kupitia yeye namna hii, aseme, "Huyo hapo Roho Wangu akibubujika apendavyo. Huyo hapo. Huyo, huyo, na—naweza kufanya kazi." Hapa, mlete mwingine hapa na kumweka mahali pake, "Naweza kumweka mahali pake." Kufanywa wana wenye mamlaka, kuwekwa mahali pako, kudhihirishwa, anamchukua toka hapa na kumfanyia sherehe, anamtembelea na Malaika, anamwambia jambo fulani. Sasa, kama ameambiwa kweli! Sasa kama yeye anajifanya tu kitu fulani, halitafanikiwa. Hapana, la, hilo—hilo halitafanikiwa, tumekuwa na mengi sana ya hayo. Lakini namaanisha—bali namaanisha madhihirisho ya wana wa Mungu, wakati Mungu anajidhihirisha Mwenyewe na kumtuma. Na kisha anakwenda huko, na yale anayosema ni Kweli. Anayofanya ni Kweli. Anachofanya, humdhihirisha Kristo. Unampimaje? Kwa jinsi anavyodumu na Neno, moja kwa moja na Neno. Unaona, hivyo ndivyo mnavyowajua watu wote, ni kwa jinsi anavyodumu na Neno. "Kama hawasemi kulingana na Neno, hamna Uzima ndani yao," inasema Biblia. Unaona? Waacheni.

88 Sasa hebu tusome, ndipo ita—itatubidi kumaliza, kwa kuwa muda wetu unakwisha. Vema, katika ana ya 10, ama aya ya 9, hasa.

*Akisha kutujulisha siri ya mapenzi yake,* apate kutufanya wana wenye mamlaka, *sawasawa na uradhi wa mapenzi yake aliyokusudia katika yeye huyo.*

Yeye alikusudia hili Mwenyewe, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ni wangapi wanaofahamu jambo hilo? Unaona?

*Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu …*

Loo, jamani, tumewasili tena! A-ha! Loo, hebu—hebu—hebu tulipite tu, unaona.

*… madaraka ya wakati makamilifu …*

89 Je, unaamini katika majira? Biblia ilisema hivyo, "Kuleta madaraka ya wakati mkamilifu." Utimilifu wa wakati ni nini? Kumekuwako na wakati wa, vema, kulikuwako na wakati wa Torati ya Musa. Kulikuwa na wakati wa—wa—wa Yohana Mbatizaji. Kulikuwa na wakati wa Kristo. Kulikuwa na wakati wa madhehebu ya kanisa. Kulikuwa na wakati wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu. Sasa ni wakati wa kufanywa wana wenye mamlaka, kile ulimwengu unachotazamia, unaugua. "Na hapo wakati wa utimilifu utakapokuja,

hapo wakati wa utimilifu wa wakati." Utimilifu huo wa wakati ni nini? Wakati wafu watakapofufuka, wakati magonjwa yatakapokoma, wakati ninii … wakati dunia yote itakapoacha kuugua. "Utimilifu wa wakati mkamilifu." Angalia jambo hili.

> Ambapo *kuleta madaraka ya wakati mkamilifu, atavijumuisha vitu vyote katika Kristo, …*

Hivi hamna furaha? Atafanyaje jambo hilo? Atavijumuisha vitu vyote katika Nani? [Kusanyiko linasema, "Kristo." — Mh.] Unaingiaje katika Kristo? ["Kwa Roho mmoja."] Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika ["Mwili mmoja"] Mwili mmoja. Na Mwili huo ni Mwili wa Nani? ["Wa Kristo."] Umehukumiwa tayari. ["Amina."] Yeye alichukua hukumu yetu. Basi sisi ni nini? "Nitakapoiona ile ["Damu."] Damu, nitapita juu yako." Kila wakati anapouangalia ule Mwili, Huo hapo umekaa pale, umetapakaa damu. Nimo mle jinsi gani? Kwa Roho Mtakatifu. Yeye hupita tu. Loo, jamani!

> Na wakati wa utimilifu wa wakati mkamilifu, apate kuvijumuisha … *vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni, …*

90 Sasa kama ukitaka kuzungumza juu ya jina, tutaanzia nalo sasa hivi kwa muda kidogo. Familia yote Mbinguni inaitwa nani? [Kusanyiko linasema, "Yesu Kristo." — Mh.] Familia yote duniani inaitwa nani? ["Yesu Kristo."]

Kuna wanawake wazuri hapa, wazuri, matajiri, bibi halisi, mabibi. Kuna Bibi Branham mmoja, Bibi William Branham, yeye ni mke wangu. Ndiye anayeenda nyumbani pamoja nami. Mnaona, ninyi wengine mnaenda pamoja na waume zenu.

Kuna Kanisa moja kuu lililo hai la Mungu aliye hai, linaitwa Jina Lake, limejazwa na Roho Wake. Hiyo ni kweli. Sisemi …

91 Mimi silaumu kazi nzuri, siyalaumu mahospitali yao na mambo mazuri wanayofanya. Nafikiri hilo ni zuri sana, na ni baraka za Mungu kwa binadamu walio maskini na wanaoteseka. Siyahukumu mambo haya mengine yote wanayofanya. Sawa, hilo ni sawa tu. Na madhehebu yao makubwa na mamilioni ya dola, ni bora nione hayo badala vilabu vyapombe pembeni, wakati wo wote. Hakika ninawaheshimu kama wahudumu wakisimama mimbarani.

Lakini inapofikia kule kukusanyika pamoja mwishoni mwa wakati, itakuwa na kutazamia madhihirisho ya wana wa Mungu, katika wakati huo … apate kuwakusanya wote pamoja, wote walioletwa wakaingizwa katika Kristo. Kristo ni nini? Ni wangapi … Tunaingiaje ndani Yake? I Wakorintho 12, "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, ambao ni Mwili wa Kristo, na kufanywa washirika wa kila kipawa na kila kitu chema alicho nacho." Sivyo? "Na dunia yote inaugua, inalia, ikitazamia madhihirisho ambapo Kristo na Kanisa Lake wataungana pamoja."

> *Yaani … kuleta madaraka ya wakati wa mkamilifu … vijumuisha … …* vyote *katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia; Naam, katika yeye: … dunia; na hata katika yake:*
>
> *Na ndani yake …* tumepata *urithi, …*

92 Loo, Ndugu Neville, nisamehe kwa kuchukua wakati huu. Mimi … hilo neno "urithi." Loo-loo-loo-loo! Loo, halina budi kufanya hivyo! Loo-loo-loo-loo! Najua Yeye … Ni Jamaa yangu aliye wa jkaribu. Mimi si … Natumaini mimi sina wazimu. Ni—ni—ninaninii tu … Sidhani nina wazimu. Lakini, loo, jamani! Kitu gani? "Urithi." Tumepata urithi. Mtu fulani hana budi kukuachia kitu fulani. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuachia kitu fulani. Jina lililoandikwa kwenye kile Kitabu, ili kwamba wakati Mwana-Kondoo atakapochinjwa utatambulika pamoja Naye. Loo! Hebu tuliache hilo kwa ajili ya usiku huu. Hebu tuendelee tu kusoma kidogo. Jamani, jamani! Tutawezaje kufikia ile aya ya 3 usiku huu, ama sura ya 3? Hata hatujasoma aya nne ama tano za hii. Sasa tunakaribia kufunga, hata hivyo, itanibidi tu kuisoma na kuiacha.

> *Na ndani yake sisi nasi tumepata urithi, huku …*

93 Nini? Tunaupataje urithi huu hapa? Tuliupataje? Kwa sababu tulitembea imara? Tunapataje urithi huu? Kwa sababu tulichaguliwa tangu zamani. Amina. Whiu! Ndugu zangu Waarmenia, najua jambo hilo ni gumu sana. Sikusudii kuumiza, lakini inanifanya nijsikie vizuri sana kujua ya kwamba ina … U—u—unao, uo, ndugu, vema. Ni kwamba tu huuoni. Unao hata hivyo. Unaona? Huna neno, unaona, uko sawa. Unaona? Lakini, loo, bali huo ni mzuri sana ukiutazama. Ndiyo. Ni kama tu vile Ndugu Neville alivyosema juu ya njia yenye nguzo na matao juu yake, "Jitwalie ngaz yenye vipandio uende kule ujionee kilichoko." Naam, bwana. Hivyo ndivyo Hii ilivyo. Roho Mtakatifu wa Mungu ndiye ngazi yetu yenye vipandio kutuambia tulicho nacho. Unaona?

94 Mnaona, urithi. Loo, jamani! "Ukiwa …" Ni urithi wa namna gani?

> *… huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye ambaye hufanya*

*mambo yote kwa shauri la mapenzi yake;*

Wakati Yeye alipokuwa … kabla Yeye hajawa Baba, kabla hajawa Mungu, kabla hajawa Mwokozi, kabla ya kuwa Mponyaji, kabla ya mambo yote, Yeye alitangulia kuchagua, akaweka Jina la Mwana-Kondoo kwenye Kitabu, akaangalia chini kwa kujua Kwake tangu awali na kuliona jina lako, akaliandika mle pia. Ni kitu gani? Na baada ya kitambo kidogo tukaja ulimwenguni, tumezaliwa na wazazi wenye dhambi; tunatembea kote ulimwenguni, mwajua. Muda si muda, kama yule maskini Myahudi mwenye pua kama ndoana, Paulo, mwajua, na—naye alikuwa akitekeleza, na, muda si muda, Kitu fulani kikasema, "Basi, basi, basi, basi!"

Unasema, "Loo, Aba, Baba!"

Na hapa sisi tunaanza kuja, unaona. Alituchagua tangu zamani kwa ajili ya urithi wetu katika Yeye, uliochaguliwa tangu zamani kwa ajili yetu. Unaona, tuliurithi kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Unaona? Loo! Kwa ajili ya kusudi Lake Mwenyewe kutekeleza mapenzi Yake Mwenyewe mema, hiyo ni kweli kabisa, kuwa Mungu na Mwokozi.

*Nanyi pia mmekwisha kumwamini huyo,* baada ya *kulisikia neno la kweli, …*

95 Basi ni Nani aliye Kweli? Yesu ndiye Kweli, Kweli ya Injili. Injili gani? Kuna Injili moja tu. Wagalatia 1, ilisema, "Hata Malaika akihubiri Injili nyingine yo yote, na alaaniwe." Hii ndiyo Injili, Injili ya wokovu wenu; si nyingine, hakuna nyingine. "Hakuna—hakuna jina lingine walilopewa chini ya Mbingu ambalo kwalo wanapaswa kuokolewa." Bali katika Jina la nani? [Kusanyiko linasema, "Bwana Yesu Kristo." — Mh.] Loo, mie!

*… ambaye ndani yake … tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri …*

Loo, "Mkiisha kuamini!" Tunawezaje kuvuka hilo, ndugu? Hebu tuiache tu kwa ajili ya usiku wa leo, mnasemaje? Loo, jamani! Si—siwezi tu kwenda te—tena mbele zaidi ya hapo. Hebu tuliache kwa ajili ya usiku wa leo. Siwezi tu kuacha neno hilo "kutiwa muhuri," jinsi unavyoingia mle, unaona.

96 Urithi kwa njia ya kuchaguliwa tangu zamani. Mimi nilirithi kitu fulani. Urithi gani? Ilipasa kuwepo na mtu fulani atakayeniachia urithi. Mbona, unasema, "Yesu alikuachia urithi." Ati nini? Yesu hakuniachia urithi, Yesu hakukuachia urithi; Yeye alishuka tu akaja akalipia urithi wako, akakuleta kwenye urithi wako. Lakini jina lako liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu ndiye aliyekupa urithi wako. Urithi wako ndio ulikuwa wa kwanza. Yesu alikuja tu … Mengi, hivi ndivyo wanavyojaribu kufanya jambo hilo, "Mungu akisema, 'Vema, kuna watu wengi sana waliopotea. Hakuna hata mmoja wao atakayeokolewa, kwa hiyo nitamtuma Yesu na huenda ikawa Yeye ataninii … mtu fulani atamsikitikia, na ajue yale niliyofanya naye ataokolewa.'" Loo, rehema! Nisingeweza kuendesha kazi yangu namna hiyo, hata ingawa naiendesha vibaya jinsi gani wakati mwingine. Unaona? Si—nisingefanya jambo hilo hivyo. Vipi kuhusu Mungu?

97 Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, aliona kabisa ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa, Yeye alimtuma Yesu kuwaokoa wale ambao tayari alikuwa amewachagua. Je, Paulo hakusema, aya tano zilizotangulia hii, ya kwamba "Yeye alituchagua katika Yeye kabla hata ulimwengu haujakuwako"? Huo ndio urithi wetu. Mungu alituchagua, na kumwacha Yesu aje na kulipa ile gharama. Hiyo ni nini? Kumwaga Kwake Damu Yake, ili kwamba tusihesabiwe dhambi yo yote. Hufanyi lolote. Lakini kama wewe …

"Yeye atendaye dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu."

Sasa, na hapo ndipo utakapoinuka tena, useme, "Vipi kuhusu hilo, Ndugu Branham?"

Lakini kumbukeni tu, mnaona, "walioupokea *ujuzi* wa ile Kweli." Wao hawakuipokea ile Kweli kamwe, walipokea tu ujuzi Wake. Unaona? Haiwezekani kwa wale waliokwisha kupewa nuru na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, wakazionja nguvu za Neno zuri. Kama hao waamini wakwamia mpakani kule nyuma. Wengi sana wameniandikia barua juu ya jambo hilo.

98 Hao waaminio wakwamia mpakani walienda moja kwa moja wakafika pale, Yoshua na Kalebu walivuka moja kwa moja kule. Kwa nini? Sasa tutaiita hiyo Roho Mtakatifu, ile nchi huko kule. Hawa hapa wanarudi *hapa*. Ama hapa *juu*, tuseme *hii* ni Roho Mtakatifu, nao wako nyma *hapa*, unaona. Hapo ndipo penye ile ahadi, *pale*. "'Vema, kama wangewatuma wapelelezi kumi, mmoja kutoka katika kila kabila, kusudi sisi makabila yote tuweze kujua urithi wetu ni nini, ambapo wote watapewa sehemu yao, mahali tutakapowekwa.' Kwa hiyo, nitawatuma wapelelezi."

Hao wote wakafika kule, "Loo, jamani! La. Tungeitwa watakatifu wanaojiviringisha, tangu wakati huo na kuendelea. La, a-ha, tusingeweza kufanya hivyo." Unaona?

Yoshua na Kalebu wakasema, "Nitaona jinsi ilivyo." Kwa hiyo wakaja huku na kuangalia kila mahali. Jamani, walinyosha mikono yao kule juu wakakata kishada kikubwa cha zabibu zao nao wakashuka wakarudi. Kasema, "Jamani, ni nzuri, ni nzuri tu! Hii, hebu onja baadhi yake, ni nzuri hasa!"

"Loo, hizo ni nzuri, lakini, loo, hebu waangalie hao majitu … Loo, tusingeweza kufanya jambo hilo. Kuwa kinyume na hayo madhehebu yote makubwa, vitu hivyo vyote vikubwa? Loo, ni vibaya sana, hatuwezi kufanya hivyo. La, bwana! Haidhuru ni nani, hatutafanya hivyo. La, bwana." Nao wakaanza kusema, "Loo, hebu turudie zile sufuria za nyama za Misri. Ni afadhali hata tungalikaa huko. Hatuwezi kufanya jambo hilo, barabara hii ni nyembamba sana. Tunajua hatuwezi kufanya *hivi*, hatuwezi kufanya *vile*."

99 Mzee Kalebu akasema, "Tulieni, ninyi nyote!" Yoshua akasema, "Nyamazeni, kila mmoja wenu! Hebu niseme jambo fulani."

"Loo, ole, ole, ole, hatuwezi kufanya hivyo! Loo, tusingeweza. Vema, kama ilinibidi kuacha karamu yangu ya kadi, Ndugu Branham! Kama itanibidi kuacha nywele zangu zikue kama za mwanamke fulani mzee, hata sijui la kufanya. Kama ikinibidi kuvua kaptura yangu ndogo, si—si—mimi, jamani, nisingeweza tu, unajua. Na kama ningeachana na misokoto yangu, kama ilinilazimu kufanya hivyo!" Ewe maskini mfano uliotolewa. Naam. "Siwezi kufanya hilo kabisa."

Yoshua akasema, "Loo, ni nzuri. Haleluya! Tunaweza kuitwaa." Ilikuwa nini? Walikuwa wakiangalia hiyo miji mikubwa iliyokuwa imezungushiwa kuta. Na Yoshua na Kalebu walikuwa wakitazama ahadi aliyoitoa Mungu. Dumu na Neno, haidhuru wewe ni nani. Dumu na Neno!

100 Kwa maana Petro alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu," (Nchi gani ya ahadi?) "Na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

Usiache jambo hili likuumize, tukifunga, tafadhali usiudhike. Unaona? Hapo ninyi Wapilgrim Holiness na Wanazarayo, mliingia moja kwa moja katika utakaso, mkapada moja kwa moja mpaka mahali ambapo hata mngeweza kuziona zabibu, kisha mkageuka na kurudi. Mnaona kilichotukia? Hiyo ndiyo shida, hamkwenda hata mkaingia nchini. Nionyeshe Mnazarayo mmoja ama Mpilgrim Holiness, ama ye yote wao aliye nchini leo, anayeendesha mikutano mikubwa ya uponyaji huku zikifanyika ishara na maajabu. Nionyeshe mmoja. Mmetulia Misri, mkazirudia kwenye sufuria za vitunguu saumu. Mlikomea Kadeshi-barnea. Hiyo ni kweli.

101 Angalieni, na hebu niwape fungu lenu, katika Waebrania sura ya 6. "Kwa maana haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru," mlijua vizuri zaidi. Kama haujui, mnalijua sasa. Unaona? "Na kufanywa washirika, na kuvionja vipawa vya Mbinguni."

Kuonja, unaona. Watu huenda kanisani, na kuketi pale na kusema, "Unajua, hao, wanaweza wawe sahihi. Hiyo—hiyo—hiyo ingeweza kuwa sahihi. Huenda ikawa vile vile tu, lakini nakuambia, ewe kijana, inahitajika imani nyingi sana kufanya jambo hilo."

"Wakaonja vipawa vya Mbinguni, na wameihesabu ile Damu ya agano kuwa ni 'kitu ovyou,' ambayo mlitakaswa kwayo."

Kama vile mhubiri, mama yake anamtuma. Yeye anasema, "Nimepata wito wa kuwa mtumishi wa Bwana."

"Vema. Jambo la kwanza ninalopaswa kufanya ni kuwa dobi, mpenzi, nami nitakupeleka shule fulani." Jambo baya sana alilopata kufanya. Hiyo ni kweli. Wataondoa yote ndani yake ambayo Mungu anajaribu kuweka ndani yake. Basi, sasa angalia.

102 "Kwa maana kama tukitenda dhambi kusudi, tufanye dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, ujuzi. Tuuone katika Maandiko na kujua kwamba Biblia inasema ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kuona jambo Hilo, ni ujuzi wa ile Kweli. Tukiuona, tunakataa, na kuihesabu ile Damu ya agano …"

Mtu fulani anasema, "Loo, naam, ninaamini Mu-Mungu." Vema, wewe unapiga hatua ya kwanza.

"Hakika, ninaamini katika utakaso." Vema, wewe uko mpakani, papa hapa tayari kumpokea Roho Mtakatifu. Lakini unaangalia kule na kusema, "Si—si—sijui kitu juu ya jambo hilo. Kama itanibidi kutenda kama … La. Sijui. Unajua jinsi wanavyowaita hao watu? A-ha, sijui kama ningeweza kufanya hivyo ama la. La, naamini nitaendelea tu na kujiunga …?…" Unaona? Unaona?

Nanyi mnajua kinachotukia? Yeye alisema, "Haiwezekani kwao kuingia kamwe." Wameitenda dhambi hata siku yao ya neema ikaisha. Biblia ilisema hivyo. Najua hilo ni kali, lakini Biblia ilisema, "Wameonja vipawa vya Mbinguni, na kuihesabu Damu ya agano ambayo kwayo…"

103 Wao wanasema, "Naamini katika utakaso, maisha mazuri, yaliyo safi, matakatifu."

Hakika, lakini wewe, ulipouona ubatizo wa Roho Mtakatifu, na ubatizo na mambo haya mengine yote katika Biblia, nawe umefanya nini? Umeihesabu Damu ya agano ambayo kwayo ulitakaswa, "kitu ovyo." Ni kitu gani ulimwenguni kilichokupeleka kule, ewe mtu? Nini …?… Ni kitu gani kilichokuzuia kuwa mwenye

dhambi mbaya sana? Ni kitu gani kilichoondoa dhambi maishani mwako, na kuvuta sigara na kunywa pombe, na wanawake na kadhalika maishani mwako, mambo ambavyo hayangepaswa kuwepo? Ni kitu gani kilichosaababisha hayo? Ile Damu ya agano! Ndipo ukakaribia sana kuonja kuonja zabibu kutoka Nchi ile nyingine, na ukaionea Injili haya, unaliogopa dhehebu lako! Mungu akurehemu! Naam, bwana. "Wakaihesabu Damu ya agano kuwa 'kitu ovyo,' na kuifanyia jeuri kazi za neema. Haiwezekani kwake kuingia katika ile Nchi."

104 Ni kitu gani kilichotukia? Ninawauliza. Sasa, mimi ni mtu wa mifano, na mtu ye yote anayeijua Biblia ni mtu wa mifano. Je! kuna mmoja kati ya watu hao aliyewahi kuingia katika nchi ya ahadi? Hakuna hata mmoja wao. Ni nani waliofaulu, ni akina nani walienda kule? Wale waliotangulia kwenda, walirudi na kusema, "Tunaweza kuitwa, tunaweza kumpoea Roho Mtakatifu kwa maana Mungu alisema hivyo! Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, kama mimi 'ningetubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo,' ningempokea Roho Mtakatifu, ahadi ni kwa ajili yangu. Niko tayari kufanya hivyo. Yangu, hiyo ahadi ni yangu." Mnalipata? "Sasa ahadi hii ni yangu. Ninaupokea, ni yangu. Hakika ni yangu." Walikuwa hao peke yao.

"Loo," unasema, "lakini, Ndugu Branham, katika ufufuo!" Wao hawatakuwapo. "Loo, ati hawatakuwepo?" La, bwana. Yesu alisema.

105 Wao walisema, "Nawe unajifanya mkubwa kama Musa, na Wewe ulisema ulikuwa hivyo, Wewe 'ulimwona Ibrahimu.'" Naye akasema, "Na—na—na—na Ibrahimu amekufa kitambo! Mbona, Wewe hu—Hunajapita bado umri wa zaidi ya miaka hamsini, Nawe ulisema ulimwona Ibrahimu?"

Yeye akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Loo, jamani! Yule "MIMI NIKO," aliyeko daima, Mungu wa Milele. Sio jana, si kesho, "MIMI NIKO." Unaona? Mungu aliyeko daima, Elohimu, "MIMI NIKO." Ndipo wakaokota … Walikuwa wakitaka kumwua wakati huo.

Wakasema, "Vema, baba zetu walikula mana jangwani kwa muda wa miaka arobaini. Mungu alinyesha mkate moja kwa moja toka Mbinguni na kuwalisha. Wao walienda kanisani na walikuwa wafuasi wazuri wa kanisa kwa muda wa miaka arobaini. Mama yangu mzee alikufa papa hapa katika hili kanisa," na kila kitu namna hiyo. "Baba zangu walikula mana jangwani kwa muda wa miaka arobaini."

Naye Yesu akasema, "Na kila mmoja wao amekufa." *Kufa* humaanisha "kutengwa Milele." "Kila mmoja wao amekufa. Lakini Mimi nawaambia, ya kwamba Mimi ndimi Chakula cha Uzima kishukacho kutoka Mbinguni kwa Mungu. Mtu akila Mkate huu wa Roho, ana Uzima wa Milele wala hawezi kuangamia. Nami nitamfufua katika siku ya mwisho." Loo, ndugu, hivi Yeye si wa ajabu?

Yeye si ni wa ajabu, wa ajabu, wa ajabu?
Yesu si Bwana wetu si ni wa ajabu?
Macho yameona, masikio yamesikia, yale yaliyoandikwa katika Neno la Mungu;
Yesu si Bwana wetu si ni wa ajabu?

106 Je, hiyo ni kweli? Tunaona Roho Wake wa upambanuzi akipitia katikati yetu. Tunamwona akifanya miujiza na ishara na maajabu. Tunalisikia limeandikwa moja kwa moja kutoka kwenye Neno hapa, na kuliona likihakikishwa moja kwa moja pale. Loo, jamani!

Macho yameona, masikio yamesikia, yale yaliyoandikwa katika Neno la Mungu;
Yesu si Bwana wangu si ni wa ajabu?

107 Katika dakika nyingine mbili, ama tatu, kutakuwa na ibada ya ubatizo wa maji itakayofanyika hapa. Na sasa wale watakaobatizwa, hebu wanawake waende *huu*, na wanaume upande *huu*. Na sasa wanaume kwenye upande wangu wa kushoto, upande *huu*. Nao wanawake upande *huu*. Kutakuwa na akina dada mle ndani wakiwa na nguo tayari. Na kama mwanamume yeyote au mwanamke yeyote hapa asubuhi ya leo, ambaye ameshawishika kwamba unaamini Neno la Mungu, nawe unaamini ya kwamba Mungu hutimiza ahadi Yake, ya kwamba kama mtu atatubu dhambi zake zote … Sasa, Damu haijafanya kitu bado. La, ni imani yako tu katika Mungu. Na Mungu anaita, tu, "Phew, phew, phew!" akikuita, hilo ndilo analofanya sasa, "Phew, phew!"

"Sijawahi kubatizwa."

"Phew, phew!"

"Vema, vema, laiti ningalianza na kufanya jambo tofauti."

"Phew!" Jambo, jambo ndilo hilo, anza, ndipo—ndipo utakuwa tofauti baada ya kuanza kwako. Unaona? Huna budi kugeuka, uanze, unaona.

Unasema, "Vema, si—si—sijaliona hivyo hasa."

108 Vema, ndugu mpendwa, nataka unionyeshe Andiko moja ambapo mtu ye yote … Nimetoa maneno haya kwa muda wa miaka thelathini na moja ya huduma kote ulimwenguni, mbele ya maaskofu na

kadhalika, ambapo mtu mmoja, mtu mmoja aliwahi kubatizwa kwa njia nyingine yoyote isipokuwa kwa Jina la Yesu Kristo. Na kila mtu ambaye hakubatizwa katika Jina la Yesu, ilimbidi aje na kubatizwa tena katika Jina hilo.

Mungu alikuwa na Jina moja tu, na Jina Lake ni Yesu. Huyo alikuwa Mwanawe, alichukua Jina la Mwanawe. Mungu! Sasa, Yesu, ule mwili ulikuwa mtu. Tunajua jambo hilo. Huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu aliyekuwa ametiwa uvuli. Sasa sisi hatuamini katika ule mfano wa umoja, hao watu wanaosema ya kwamba Mungu ni kama kidole chako. Tunaamini kuna si… sifa tatu za Mungu. Sifa tatu za Mungu, Mungu alidhihirishwa kwazo. Lakini kuna Mungu mmoja. Unaona? Hiyo ni kweli. Hatuamini … Tunaamini katika—katika … Hebu niseme hivi, tunaamini ya kwamba Mungu aliishi katika ofisi tatu. Alikuwa na ofisi duniani wakati mmoja.

109 Sasa, ninyi wanawake nendeni upande *huu*, nanyi wanaume nendeni upande *huu*, mnaojitayarisha. Nao wanajitayarisha kwa ajili ya ibada ya ubatizo sasa.

110 Na, sasa, Mungu alikuwa na ofisi tatu. Moja iliitwa Ubaba, ama kipindi cha Baba; hiyo nyingine iliitwa Mwana; na hiyo nyingine iliitwa Roho Mtakatifu. Sasa, leo, ni—ni majira gani ambayo Baba anafanya kazi leo? [Kusanyiko linasema, "Roho Mtakatifu." — Mh.] Roho Mtakatifu. Yeye alikuwa nani katika siku zilizopita? ["Yesu."] Yesu. Alikuwa nini katika siku zilizotangulia hizo? ["Baba."] Lakini ilikuwa tu ni Mungu mmoja tu! Sivyo? Yeye ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Hizo tatu, hizo ofisi tatu za Mungu mmoja. Mungu mmoja!

Lakini sasa, Baba si jina, sivyo? Nataka kuwaulizeni. Sasa nataka kuwapa Mathayo 28:19, ambapo Yesu alisema, "Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkawabatize kwa Jina, " (J-i-n-a) "Jina la Baba …"

111 Sasa nataka kuona jinsi mnavyojua Maandiko yenu vizuri. Niambieni nitakapotoka nje. Naye akawaambia, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitawafuata hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo,"(hayo yote ni kweli?)"Watanena kwa lugha mpya, watashika nyoka." Sasa nitawanukulieni, Mathayo …

Sasa sikilizeni. Namwuliza mwanahistoria ye yote. Sasa haya yako kwenye kanda, hizi zinazunguka ulimwengu mzima. Namwomba mwanahistoria yeyote aje kwangu aniletee fungu lo lote la Maandiko, fungu lo lote la … ama si Maandiko, fungu lo lote la Maandiko au historia yo yote, aya yoyote ya historia ambayo iliwahi kuonyesha ya kwamba Mprotestanti yeyote, kwamba mtu ye yote aliwahi kubatizwa kwa jina ya "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" mpaka kanisa Katoliki lilipouamrisha katika Baraza la Nikea. Sasa hayo yako kwenye kanda, zinasambazwa kote ulimwenguni, hufasiriwa katika lugha thelathini na saba. Nitakulipia gharama yako ya kuvuka bahari. Hiyo ni kweli. "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" ni fundisho la uongo, sharti haramu la Katoliki, wala si ubatizo wa Kikristo. Sawa! Luther aliuleta kutoka kwenye kanisa Katoliki, pamoja na katekismo, Wesley aliukubali kisha ukasambaa. Lakini hii ndiyo siku ya kudhihirishwa kwa wana wa Mungu, wakati zile siri zilizofichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu zitajulikana. Hii ndiyo ile saa. Hakika.

112 Kumbukeni, hakuna mtu kamwe katika Biblia aliyewahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Kwa miaka mia tatu baada ya kifo cha mtume wa mwisho, hapakuwa na mtu aliyewahi kubatizwa kwa jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Wao walikuwa … Nimesoma *Mababa Waliotangulia Nekea*, *Baraza la Nikea*, na kutoka hapo wameunda kile wanachoita "kanisa la Kikristo la ulimwenguni kote" na kuunda dhehebu kutokana na hilo na kuwalazimisha watu wote kujiunga nayo, ambalo lilikuwa kanisa Katoliki. Neno lenyewe *katoliki* hasa linamaanisha "ulimwengu wote," kanisa la Kikristo la ulimwenguni kote, ulimwenguni kote, kanisa moja litakaloenea ulimwenguni. Na Ukristo huu, wanawalazimisha watu wajiunge nao. Mle ndani waliingiza, wameondoa Venus wakamwingiza Mariamu. Wamemshusha Paulo … ama Jupiter, na kumwinua Paulo. Lingali ni upagani! Sawa. Kanisa Katoliki lilitoka mle, na baada ya miaka mia tano …

113 Wana mchezo wa kuigiza unaoendelea huko Louisville sasa, wa *Ben Hur*. Walikuwa na zile *Amri Kumi* si muda mrefu uliopita. Laiti wangalicheza mmoja wa, kama wangeweza, wa ile miaka elfu moja mia tano ya zile nyakati za giza. Laiti wangalionyesha huo. Miaka elfu moja na mia tano ya mateso ya kipagani, wakati walipomlazimisha kila mtu na kuwaua, wakawaua, wakawanyonga kwa kamba. Wakamfungia maksai kwenye mkono mmoja na maksai mwingine mkono mwingine, ndipo wakawafanya aidha waubusu msalaba ama wampige mmoja aende upande huu na mwingine upande ule. Nimeuweka mkono wangu, kule Uswisi kwenyewe, nyuma ya nguzo ambako walisimama huko na kukata ndimi zao na kuwaita wachawi na kila kitu kingine. Hiyo ni kweli kabisa. Sawa!

114 Na roho yule yule anaishi leo. Ni sheria tu inayoizuia. Ngojeni mpaka itakapopata uhuru wake. Biblia ilisema hivyo. Ngojeni tu mpaka itakapoonyesha jinsi ilivyo, itakapoata nafasi ya kufanya hivyo. Huenda mkaipigia kura hivi karibuni, nijuavyo mimi. Unaona? Itakuja, itakuja. Hakuna njia ya kuizuia. Haina budi kuja. Hiyo ni kweli. Haina budi kuja, inakuja. Kwa hiyo ijapo, angalieni tu. Lakini, ndugu, inakupasa kujua

jambo hili moja, najua Yeye niliyemwamini. Haleluya! Kuendelea kutembea tu. Unaona. Hivyo ndivyo ilivyo.

115 Kuna wakati ambapo yule—wakati yule mwandishi, wakati nilipomwambia yule mwandishi wa Biblia ya Lam- … Lamsa—Lamsa, wakati alipotazama na kuona ile ishara ya kale ya Mungu, namna hiyo hasa, nukta tatu ndogo ndani yake, nikasema, "Hizo ni nini?"

Akasema, "Huyo ni Mungu katika sifa tatu."

Nikasema, "Kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?"

Akanitazama. Akasema, "Je! Unaamini jambo hilo?"

Nami nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Niliona huo utambuzi hivi majuzi usiku, nikafikiri wewe ulikuwa nabii wa Bwana." Kasema, "Mungu na aubariki moyo wako." Akanikumbatia, kasema, "Sasa najua ndivyo ilivyo." Akasema, "Hawa Wamarekani hata hawajui nini." Kasema, "Hata hawajui kitu." Kasema, "Wanajaribu kukichukua Kitabu cha Mashariki na kutengeneza Kitabu cha Magharibi kutokana na Hicho. Hata hawajui Biblia yao." Akasema, "Hakuna Jina lingine walilopewa chini ya Mbingu, hakuna Jina lingine, kwa maana kila mtu alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Hakuna kitu kama watu watatu katika Mungu mmoja." Na huyo ni Ndugu Lamsa, Daktari Lamsa, mtafsiri wa Biblia ya Lamsa, ambaye ni rafiki msiri wa Eisenhower na wanadiplomasia wote wakuu wa ulimwenguni, na wengine kadha wa kadha, akanikumbatia, kasema, "Siku moja watapiga risasi kwa ajili ya jambo hilo. Lakini," kasema,"kumbuka, watu hao wote hufa kwa ajili ya msimamo fulani."

116 Ningetaka kuwa kama wakati ule mzee Petro alipofungwa gerezani. Kulikuwa na maskini mvulana mdogo mle ndani naye alikuwa na wasiwasi sana. Naye akasema, "Loo, kuna nini?"

Kasema, "Unajua utanyongwa?"

Petro akasema, "Naam."

Akasema, "Vema, unajiandaa kufa leo."

Akasema, "Naam."

Akasema, "Vema, wao wana—wao wana … wewe huogopi?"

Akasema, "La."

Akasema, "Hapana budi wewe ni mmoja wa hao wanaowaita Wakristo."

Akasema, "Naam."

Kasema, "Kulitokea nini?"

Naye akamwambia, akaketi chini na kumsimulia hiyo habari. Na ilipokuwa ikiendelea, ikafika mahali, akasema, "Nami ningelikuwa huru asubuhi ya leo. Ningeweza kwenda na kujiunga na baadhi ya madhehebu yao na niendelee tu kuishi, mnaona. Ningeweza kuwa huru. Lakini nilipoanza kutoka kwenye lango la jiji hili, ndipo nikamwona Mtu akija, akiingia ndani. Nilijua Yeye alikuwa ni Nani. Nikasema, 'Bwana, unaenda wapi?' Akasema, 'Ninarudi kwenda kusulibishwa tena.'" Kasema, "Nikarudi moja kwa moja."

Papo hapo wakasema, "Ni nani anayeitwa Simoni Petro?"

Kasema, "Mimi hapa!"

Kasema "Tuko tayari hapa kwa ajili yako."

Kasema "Nimekuwa nikiwasubiri." Akatoka nje moja kwa moja.

Yule mvulana akamgusa begani, na kusema, "Ngoja kidogo, Simoni; nliamkubali huyo Mungu pia! Na sasa siogopi; hebu wangu ufuate." Hiyo ni kweli. Haleluya!

Inaendelea … Inadondosha damu, naam, inadondosha damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondosha damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya ile Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inaendelea kudondosha damu.
Wa kwanza kufa kwa ajili ya huu mpango wa Roho Mtakatifu,
Alikuwa ni Yohana Mbatizaji, bali alikufa kama mwanadamu;
Ndipo Bwana Yesu akaja, wakamsulibisha Yeye,
Alihubiri ya kwamba Roho angewaokoa watu mbali na dhambi.
Kuna Petro na Paulo, na Yohana mfunuaji,

Walitoa maisha yao ili Injili hii iweze kung'aa;
Walichanganya damu yao, kama wale manabii wa kale,
Kwa hiyo Neno la kweli la Mungu lingeweza kusemwa kwa uaminifu.
Kuna nafsi chini ya madhabahu, zikilia, “Hata lini?”
Kwa ajili ya Bwana kuwaadhibu wale waliotenda maovu; (Sikilizeni!)
Lakini kutakuwako na wengine zaidi watakaotoa damu ya uhai wao
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na mafuriko yake mekundu.
Inadondosha damu, naam, inadondosha damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondosha … damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya ile Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondosha damu.

Andiko moja tu kabla hatujaondoka: …

*Nao wakamwambia Petro na ... hao* wengine, *ndugu zetu, tutendeje* ili tuokolewe?

*… Petro akawaambia, Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

*Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa* hao walio *mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.*

Bwana awabariki sasa. Wakati tunapoondoka. Mnaweza kuangalia ubatizo tunapo- …?…

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7